

Mtumiaji

Jarida la habari zenyet kuwajengea uelewa watumiaji wa huduma za Nishati na Maji

ISSN 2738-9014

Toleo Na. 08 • Julai - Desemba, 2023



Baraza laongeza kasi uelimishaji watumiaji

HALIUZWI



Tupige vita wizi wa dira za maji



Kutoka Ofisi ya Katibu Mtendaji

Kwa heshima kubwa, na kwa mara nyingine tena napenda kuwaalika wasomaji wote katika toleo letu Na. 08 la Jarida la Mtumiaji kutoka kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC). Jarida hili linalochapishwa mara mbili kwa mwaka, hutoa habari mahsusini kuhusu masuala yanayomhusu mtumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Toleo hili ambalo ni la pili kwa mwaka huu wa 2023, ilimesheheni habari mbalimbali zitakazoongeza uelewa wako kuhusu kazi na majukumu ya Baraza, namna linavyofanya kazi katika kumtetea mtumiaji pamoja na Makala zingine za kusisimua zikiwemo umuhimu wa matumizi endelevu ya huduma za nishati na maji.

Katika toleo hili utajifunza na kufahamu jinsi EWURA CCC inavyofanya kazi na jamii katika kutoa elimu na kuwajengea uwezo watumiaji ili kuchangia katika jitihada za kuboresha huduma za nishati na maji nchini.

Aidha, EWURA CCC inaanmini katika maendeleo endelevu na utunzaji wa rasilimali maji kwa maendeleo endelevu. Toleo hili litakupa miongozo na vidokezo muhimu kuhusu matumizi sahihi na salama ya huduma za umeme, maji, mafuta na gesi za kupikia majumbani katika suala zima la uhifadhi wa mazingira.

Hizi ni baadhi tu ya Habari na Makala muhimu zinazogusa maisha ya Watanzania zinazopatikana katika Jarida hili.

Kwa mara nyingine tena, nitoe shukrani za dhati kwa wadau wetu mbalimbali kwa kuendelea kujielimisha kupitia chapisho hili muhimu lililosheheni Habari na Makala za kina kuhusu masuala ya watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa ujumla. Hakika hili ni mionganoni mwa majirida bora kabisa nchini katika sekta za nishati na maji.



Stella Lupimo
Kaimu KATIBU MTENDAJI



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba akisikiliza kwa makini maelezo kutoka kwa Bi Catherine Ochido, Afisa kutoka EWURA CCC, kuhusu kazi na majukumu ya Baraza alipotembelea Banda la EWURA CCC wakati wa maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mwl. Julius Nyerere.. Picha na Mpigapicha Wetu

Baraza laongeza kasi uelimishaji watumiaji

Laelimisha 100,457
Latatua malalamiko 2,267

Na Lugiko L. Lugiko, Dodoma

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limendelea kuwafikia watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ili kuwapatia elimu na kuwajengea uwezo kuhusu masuala mtambuka yanayohusu huduma za nishati na maji.

Mafanikio hayo yameelezwa katika taarifa ya utendaji kazi za Baraza kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2023.

Taarifa hiyo inabainisha kuwa, watumiaji hao wamefikiwa kuititia programu mbalimbali zinazofanywa na Baraza ikiwemo uelimishaji kupi-

tia makundi mbalimbali ya watumiaji wa huduma hizo.

Taarifa hiyo imeyataja makundi yaliyofikiwa na kuelimishwa kuwa ni pamoja na akina mama, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, makundi ya vijana, waendesha pikipi - maarufu kama "Bodaboda," watumishi mbalimbali wa taasisi za umma na binafsi, wakazi mbalimbali kuititia mikutano ya serikali za mitaa, maonesho pamoja na vyombo vya habari.

Aidha, taarifa hiyo ya kiutendaji inaonesha kuwa, jumla ya programu 327 ambayo ni sawa na asilimia 90.8 ya programu 360 zilizopangwa kufanyika katika kipindi cha Januari hadi Juni 2023 zilitkelezwa na kufikia jumla ya watu 100,457.

"Idadi hii haijumuishi wadau

wengine walipata elimu kuhusu kazi za Baraza kuititia programu 123 zilizoendeshwa na ofisi na Kamtati zake kuititia vyombo vya habari mbalimbali nchini," inaeleza sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ya kiutendaji imetaja maeneo ambayo elimu kwa mtumiaji ilitolewa kuwa ni pamoja na haki na wajibu wa mtumiaji, umuhimu wa kulipa ankara kwa wakati, kutunza miundombinu ya maji na umeme, kufichua wezi na waharibifu wa miundombinu ya maji zikiwemo mita, pamoja na utaratibu sahihi wa kuwasilisha malalamiko yao.

Akitoa ufafanuzi wa taarifa hiyo katika ofisi za Baraza jijini Dodoma, Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo alibainisha

Inaendelea Uk. 4

kuwa, kumekuwa na mwamko mkubwa wa watumiaji wa huduma kufuilia masuala yanayohusu huduma za nishati na maji, hususani kuwasilisha malalamiko yao baada ya kupata elimu inayotolewa na Baraza.

"Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2023, tumeshuhudia watumiaji wakifika katika ofisi za Baraza zilizopo mikoani kuwasilisha kero, malalamiko na changamoto wanazopitaa kuhusu huduma za nishati na maji," alisema Bi Lupimo na kuongeza kuwa, baada ya kupatiwa elimu, watumiaji wamekuwa na mwamko wa kuwasilisha malalamiko yao kwa watoa huduma na kwamba Baraza limekuwa likiwasaidia watumiaji hao kuhakikisha malakaliko yao yanapatiwa ufumbuzi.

Alisema, katika kipindi hicho, Baraza limepokea jumla ya malalamiko 2,267 ambayo ni ongezeko la asilimia 34.9 ya malalamiko 1,680 tuliyotarajia kupokea.

"Miongoni mwa malalamiko yaliyopokelewa na Baraza kwa kipindi tajwa, 1,279 yalihusu huduma za maji, 941 huduma za umeme, 35 huduma za mafuta na 12 yalihusu huduma za gesi za kupikia majumbani (LPG)," alifanua Bi Lupimo.

Aidha, Kaimu Katibu Mtendaji huyu alibainisha kuwa, malalamiko yaliyopokelewa yalitatuliwa na watoa huduma, huku Baraza likishiriki kikamilifu katika utatuzi huo kwa kushirikiana na wadau husika, zikwemo mamlaka za maji pamoja na EWURA.

Baraza laongeza kasi uelimishaji watumiaji

Alisema, Baraza linajivunia kuona Watanzania sasa wana mwamko zaidi wa kupaza sauti pindi kero zinapojitokeza katika suala zima la matumizi ya huduma za nishati na maji na hatimaye kutatuliwa kwa kero hizo.

"Kwetu sisi Baraza, haya ni mafanikio muhimu sana. Jamii inapokuwa na mwamko wa kulalamikia huduma zilizo chini ya kiwango au ukosefu wa huduma kabisa ni kiashiria kizuri, kwani kwa kufanya hivyo, watoa huduma huamka na kuchukua hatua za makusudi kutatua changamoto zinazojitekeza," alisema Bi. Lupimo.

Katika hatua nyingine, taarifa hiyo inaonesha kuwa, Baraza limeshiriki katika mikutano saba (7) ya kukusanya maoni kuhusu maombi ya mamlaka mbalimbali za maji nchini kutaka kurekebisha bei za maji.

Kati ya mikutano hiyo ya kukusanya maoni ya wadau kuhusu maombi ya kurekebisha bei ni pamoja na kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi (BARUWASA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde (MPWSSA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mam-

laka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi (LUWASA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Rombo UWSA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo (Mombo UWSA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Olkesurmet, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Loliendo (Loliendo WSSA) na Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Sumbawanga (SUWASA).

Katika mikutano hiyo, Baraza lilitoa maoni na ushauri kwa kuzingatia matakwa ya kisheria huku likisisitiza uwepo wa bei ambazo watumiaji wanaweza kuzimudu ili kuhamisha watumiaji wengi zaidi kutumia huduma hizo kihalali.

Bi. Lupimo alieleza kuwa, Baraza limejipanga vyema kuendelea na uelimishaji pamoja na uwakilishi kuhusu masuala mbalimbali ya kuhabiliti kwa mujibu wa sheria katika kipindi kinachokuja, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa huduma za nishati na maji zinakuwa bora, endelevu na zinifikika kwa watumiaji wote walio tayariki kupata huduma hizo.

Katika mpango kazi wake kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2023, Baraza limejipanga kutekeleza programu 300 za uelimishaji katika jamii kwa njia mbalimbali ikiwemo kushiriki katika mikutano ya maombi ya kurekebisha bei za huduma inayoitishwa na EWURA, ili kuendelea kuwa sauti ya wengi na kuwakilisha maoni ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA.



Ndugu Miraji Vanginothi, Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa (RCC) akitoa elimu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wauguzi iliyo fanyika tarehe 26 Mei, 2023 Manispaa ya Iringa.



Tuungane kutokomeza wizi wa dira za maji

BODI YA UHARIRI

Ms. Stella Lupimo

- Mwenyekiti/Mhariri

Geofrey Sokesia - Mhariri Msanifu
Emmanuel Chagu Paul - Mjumbe

Nuru Zuberi - Mjumbe

Anadoris Komba - Mjumbe

Wachangajia

Mwasiti Athumanzi

Amani Mbogo

Chipegwa Samwel

Lugiko Lugiko

Anadoris Komba

Nuru Zuberi

Ramadhani Kakende

Emmanuel Chagu Paul

Sakina Yusuph

Josephine Ntaumenya

Zamda Mabada

Geofrey Sokesia

Wadi Omari

Neema Nnko

Dennis Ndau

Catherine Ochido

Noela Ntiluvakule

Mawasiliano

Baraza la Ushauri la Watumiaji
wa Huduma za Nishati na Maji

Jengo la PSSSF Kambarage Tower
Barabara ya Jakaya CCM

S.L.P. 772, Dodoma, Tanzania

Simu: +255 758 829 409

Baruaapepe: info@ewuracc.go.tz

Tovuti: www.ewuracc.go.tz

Katika kuhakikisha huduma bora na endelevu za maji, tunalo jukumu kubwa la kulinda miundombinu ya maji ikiwemo kutokomeza wizi wa dira za maji.

Dira ya maji ni kifaa maalumu anachofungiwa mteja wa huduma ya maji pamoja na mambo mengine kupima kiasi cha maji anayotumia. Kifaa hiki humsaidia mtumiaji kufahamu kiwango halisi cha maji anayotumia kwa kipindi fulani ili aweze kuipia bili yake kulingana na matumizi halisi kwa kipindi/mwezi husika.

Kwa upande mwengine, dira hiyo hiyo ya maji inaisaidia Mamlaka ya Maji kwenye eneo husika kutoa ankara sahihi ki kutoka kwa watumiaji/wateja na hivyo Mamlaka hiyo kuijewka kwenye nafasi nzuri ya kupata mapato kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za uzalishaji na usambazaji wa maji hadi kwa watumiaji.

Pamoja na umuhimu wa dira za maji, hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la ongezeko la vitendo vya wizi wa dira za maji. Mamlaka kadhaa za maji pamoja na watumiaji wa huduma za maji wamekiri uwepo wa vitendo hivi viovu na vya kihalifu ambavyo siyo tu vinarudisha nyuma jithada za uboreshaji wa huduma za maji nchini, bali vimekuwa mwiba katika upatikanaji wa huduma bora kwa watumiaji wa huduma hiyo, huku zikiongeza gharama za kununua dira mpya na kuzifunga, ilhali uhalifu huo unasababisha mamlaka kukosa mapato halisi kutoka kwa wateja wake.

Tumeshuhudia Mamlaka nyingi ambazo zimekuwa zikitoza wateja wake bili za maji za kukadiria zikiwa zinapitia wakati mgumu wa kukusanya mapato na pengine kusababisha changamoto ya ongezeko la maji yanayopotea.

Dira za maji zinaweza kuwa ya malipo ya kabla ama baada ya matumizi. Kwa vyovyote vile, umuhimu wake unabaki kuwa ule kwa upande wa mitoa huduma na mtumiaji wa huduma.

Kutokana na uhumi wake, EWURA CCC imekuwa mstari wa mbele katika kushauri kuhusu umuhimu wa dira za maji kwa watumiaji, jambo ambalo hakika watumiaji wengi kote nchini wanalipokea vizuri na kufungiwa dira hizo.

Wizi wa dira za maji unadhoofisha maendeleo yetu kuelekea uhakika wa maji. Serikali ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi wake. Hata hivyo, vitendo hivi vya wizi wa dira za maji vinapunguza mapato ya Serikali na kuathiri uwezo wake wa kuboresha miundombinu yake hatimaye kudhoofisha utoaji wa huduma bora.

Tunatoa wito kwa watumiaji wote wa huduma za maji na jamii kwa ujumla kushirikiana katika kutokomeza wizi wa dira za maji. Tunasisitiza kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu yetu ya maji na kuhakikisha usalama wake. Hili litawezekana tu endapo kila mmoja wetu atashiriki katika kuwafichua wezi wote wanaoshiriki katika vitendo hivi viovu.

Tunakemea vikali uhalifu huu na kuwataka wale wote wanaojihusisha na vitendo hivi kuchacha mara moja na kuwa jamii inayokerwa na vitendo hivi itoe taarifa kwa mamlaka husika ili sheria ichukue mkondo wake kwa wahusika wote.

Tukumbuke kuwa, watumiaji wote tunao wajibu na jukumu la kuwafichua wezi wa dira za maji na miundombinu mingine ya maji kwa ujumla ambayo Serikali inatoa pesa nyingi kujengwa kwa lengo la kuboresha na kufikisha huduma kwa Watanzania wote.



Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiai wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mhandisi David Ngula (wa nne kulia) akieleza malengo ya Baraza kutembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Morogoro (MORUWASA) wakati wa ziara ya Baraza kwenye Mamlaka hiyo mapema mwezi Juni, 2023.. Picha na Mpigapicha Wetu

Uwajijikaji

Tunzeni mazingira kwa huduma endelevu za maji

Na Lugiko L. Lugiko, Morogoro

Wakazi wa mji wa Morogoro wameaswa kutunza mazingira hasa maeneo ya vyanzo vya maji ili kulinda usalama wa maji na vyanzo vyake kwa huduma endelevu za maji katika manispaa ya Morogoro na viunga vyake. Wito huo umetolewa na Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Bi. Stella Lupimo wakati wa ziara ya Baraza hilo kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Morogoro (MORUWASA) iliyofanya mwezi Juni 2023 ikijumuisha wajumbe wa Baraza hilo amba walifika katika ofisi hizo kujionea namna Mamlaka hiyo inavyotoa huduma zake.

Awali, akifafanua malengo ya ziara hiyo, Mwenyekiti wa EWURA CCC, Mhandisi David Ngula alieleza kuwa, Baraza limechagua kitembelea MORUWASA ikiwa ni moja ya watoa huduma za maji nchini ili kujionea namna inavyofanya shughuli za kuzalisha maji na kuyasambaza kwa wateja wake pamoja na changamoto inazokumbana nazo katika kutekeleza majukumu yake hayo.

"Tukiwa ni chombo cha kulinda

na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji, Baraza tumeona ni vyema kufika kujionea sisi wenye namna Mamlaka hii inavyofanya kazi ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa huduma za maji kwa wakazi wengi zaidi walio katika mtandao wa maji wa MORUWASA na namna inavyoshughililia changamoto kutoka kwa wateja wake. Nasi tutafanya tathmini kuona kama Mamlaka hii inatekeleza vyema majukumu yake na tutatoa ushauri wetu," alisema Mhandisi Ngula.

Akizungumza katika eneo la kupokelea maji na kuyatibu (treatment plant), Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Mhandishi Tamim Katakweba alilijulisha Baraza kuwa, Mamlaka yake imekuwa ikitumia fedha nydingi katika kutibu maji ili yafae kwa matumizi salama ya binadamu.

Alisema kuwa hii inasababishwa na baadhi ya watu kuchafua vyanzo vya maji hivyo kusababisha uwepo wa uchafu mwangi kwenye maji ambapo kuhitaji dawa nydingi zaidi kuyatibu ili yafae kwa matumizi salama kwa binadamu.

"Moja ya changamoto tunazozi-pata katika kuhakikisha upatikanaji wa majisafi na salama ni ongezeko la maji yaliyochafuliwa kutoka kwenye

vyanzo. Maji yanapofika kwenye mitambo yetu ya kutibu huhitaji kusafishwa kwa kiwango cha juu kabisa ili yafae kwa matumizi ya kunywa. Ikiwa maji hayo yatakuwa yamechafuliwa husababisha ongezeko la gharama za kemikali za kuyatibu," alisema Mh. Katakweba.

Akizungumzia changamoto hiyo, Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Lupimo alitoa wito kwa wakazi wa Morogoro na viunga vyake kuwa, ni muhimu kulinda vyanzo vya maji na kujiepusha na tabia ya kuvichafua vyanzo hivyo ili kuwa na huduma bora na endelevu hivyo kuipunguzia MORUWASA gharama kubwa za kutibu maji.

"Tumelezwu na uongozi wa MORUWASA kwamba moja ya sababu inayofanya shughuli ya kutibu maji kuwa ngumu na inyoongeza gharama ni uchafuzi wa mazingira. Hivyo wito wetu kwa wananchi na wanufaika wa huduma zinazotolewa na MORUWASA ni kwamba, wawe sehemu ya kuboresha upatikanaji wa majisafi kwenye maeneo yao kwa kuhakikisha kuwa, wao wenye wanakuwa sehemu ya kutunza mazingira ili kupunguza gharama za kutibu maji ambazo Mamlaka inazipata," alisitisiza Bi Lupimo.

Aidha Bi Lupimo aliongeza kuwa, kupitia ziara hiyo, Wajumbe wa Baraza wamejifunza na wanaamini kuwa, kwa mipango iliyolezwu, MORUWASA imejipanga na sasa inakwenda kumaliza kabisa changamoto za upatikanaji wa huduma za maji kwenye Manispaa ya Morogoro.

Kuhusu upatikanaji wa uhakika wa maji katika Manispaa ya Morogoro, Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Mhandishi Katakweba alisema kuwa hivi karibuni tatizo la uhaba wa maji litapungua kwa kuwa Serikali inaendelea kufadhili miradi mbalimbali ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo.

"Tunawaahidi na tumelieleza Baraza kwamba Serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 26 kwa ajili ya miradi ya haraka ikiwemo mradi wa Mguru-wa-Ndege ambao tunataraja kufikia Desemba mwaka huu 2023 utakuwa umekamilika na wananchi wataanza kutumia maji ya mradi huo," alihitimisha Mhandisi Katakweba.

“EWURA CCC na Wananchi” yazidi kuelimisha umma

Uelimishaji



Na Mwandishi wetu, Kagera

Maja ya kazi inayofanywa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) ni kuhakikisha elimu kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibithi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inasambaa katika jamii yote nchini.

Ofisi ya EWURA CCC mkoa wa Kagera kwa kutambua hilo, imetengeneza mahusiano mazuri na wadau wa vyombo vya habari hususan vituo vya radio ambapo kupitia ushirikiano uliopo kati ya EWURA CCC na radio Mbiu (Sauti ya Faraja), umezaa kipindi cha “EWURA CCC na Wananchi” mnamo mwaka 2019. Ni miaka minne sasa tangu kipindi hicho kianzishwe amba-cho huruka hewani kila siku ya Ijumaa

saa 6:15 hadi saa 7:00 kamili mchana na marudio ni kila siku ya Jumapili saa nne usiku.

Akizungumza katika ofisi za EWURA CCC Kagera, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala (EWURA CCC) mkoa wa Kagera Bi. Anadorice Komba alisema kuwa kipindi cha “EWURA CCC na Wananchi” kimekuwa moja ya njia ya kufikisha elimu katika jamii juu ya huduma za nishati na maji.

“Radio Mbiu imekuwa msaada wetu mkubwa katika uelimishaji kwa umma. Kila Ijumaa ninafika redioni na kuwasilisha mada juu ya huduma za nishati na maji na wananchi wanapatna nafasi ya kuiliza maswali moja kwa moja,” alisema bi Komba.

Bi Komba alisema, kipindi hicho kimekuwa kikisikika na wanachi waishio ndani ya Manispaa ya Bukoba na maeneo mengine ya mkoa wa Kag-

Afisa Huduma kwa Wateja msaidizi na Utawala Bi. Anadorice Komba akitoa elimu juu ya huduma za nishati na maji katika kipindi cha “EWURA CCC na Wananchi” kupitia Radio Mbiu (Sauti ya Faraja) iliyopo Bunena, Manispaa ya Bukoba.
Picha na Mpigapicha Wetu

era na mikoa ya mbali na jirani kama vile Kigoma, Tabora na Dar es salaam.

“Tumekuwa tukipokea simu kutoka mikoa mbalimbali kama Dar es Salaam, Kigoma, Tabora na maeneo mengine ya nchi, hivyo inaashiria kuwa ujumbe kuhusu Baraza na kazi zake na masuala yote yanayohusu watumiaji wa hduma za nishati na maji unawafikia Watanzania wengi,” aliongeza Bi Komba.

Alivisihi vyombo vingine vya

Inaendelea Uk. 8



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SHINYANGA
(SHUWASA)



PATA TAARIFA SAHIHI NA HUDUMA BORA KUPITIA MITANDAO YETU YA KIJAMII



Huduma kwa wateja

BURE 0800711102



shuwatsa on ista



Shuwasa Shinyanga



www.shuwasa.or.tz



Shinyanga Shuwasa

SUBSCRIBE



SHUWASA TV

Tupo

Kukuhudumia



BURE 0800711102



Shuwasa Shinyanga



www.shuwasa.or.tz

“EWURA CCC na Wananchi” yazidi kuelimisha umma

habari mkoani Kagera kutoa ushirikiano zaidi kwa EWURA CCC kote Tanzania Bara kwa kuwaalika maofisa walioko mkoani humo kushiriki kwenye vipindi mbalimbali hasa vinavyohusu masuala ya huduma za nishati na maji ili kutoa elimu kuhusu huduma zinazodhibitiwa na EWURA kwa kuwa kufanya hivyo kunasaidia kuwajengea uwezo wananchi kulifahamu Baraza kama chombo chao cha utetezi na hata kukitumia kunapokuwa na uhitaji.

Akielezea kunufaishwa na kipindi cha “EWURA CCC na wananchi,” bwana Benetius Sweetbert mkazi wa kijiji cha Kyashenge kilichopo wilaya ya Muleba ambaye ni msikilizaji mzuri wa kipindi hicho alisema kuwa, kupitia kipindi hicho ametambua haki zake na namna ya kuwasilisha malalamiko kwa watoa huduma pindi akiwa na changamoto.

“Kwa kweli kupitia kipindi hiki, tumepata ufahamu mzuri kuhusu huduma za nishati na maji. Katika kijiji chetu cha Kyashenge, wananchi wengi tulifanya malipo ya kuunganishiwa huduma ya

umeme toka mwishoni mwa mwaka 2021 lakini hatukufungiwa umeme kinyume na maelezo yaliyomo kwenye Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO ambaao tulikuwa hatuufahamu, lakini kupitia kipindi hiki, tulipata uelewa juu ya mkaataba huo, na tulifuata taratibu za kulalamika hadi EWURA na tulifanikiwa kupata umeme, hivyo tunaishukuru sana EWURA CCC na Radio Mbiu,” aliezea ndugu Sweetbert.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Kagera bwana Najim Bwanika aliezea kuwa, wakati Baraza kupitia Kamati yake mkoani Kagera inaanza kutoa elimu kupitia redio Mbiu, Kamati hiyo haikujua kama elimu ya mtumiaji kupitia kipindi cha “EWURA CCC na Wananchi” kingewafikia watumiaji nje ya Manispaa Bukoba.

“Kipindi cha “EWURA CCC na Wananchi” kimewaelimisha wadau wengi kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu watumiaji wa huduma za nishati na maji ya Manispaa Bukoba.

ikiwa ni Pamoja na kufahamu haki na wajibu wao, namna ya kuwasilisha malalamiko kwa watoa huduma, pamoja na namna nzuri ya kutumia huduma hizo kwa maendeleo endelevu,” aliezea ndugu Bwanika na kuongeza kuwa, “kupitia kipindi hicho, Baraza limepokea malalamiko mengi kupitia Kamati yake na hii inaonesha ni kwa namna gani jamii imeelewa maudhui ya kipindi chetu. Sambamba na hilo, kupitia kipindi hicho Baraza limekuwa likipokea maswali, maoni na ushauri kupitia namba ya simu ya ofisi hata baada ya kipindi kuisha. Lakini pia wasikilizaji wa kipindi hiki wengine wamekuwa wakitembelea ofisi zetu kwa msaada zaidi,” alisema bwana Bwanika.

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kagera, itaendelea kutoa elimu kupitia kipindi hiki kwa sababu inaanmini watumiaji wengi zaidi watafikiwa na kuendelea kuli-tangaza Baraza na kazi zake.

Walia na huduma mbovu za maji mashulenii

Na Rose Kanango na Sakina Yusuf, Kigoma

Baadhi ya walimu wa shule za msingi Manispaa ya Kigoma Ujiji wamelalamikia ukosefu wa huduma ya maji uliosababishwa na kukatwa kwa mabomba yanayopeleka maji kwenye shule hizo.

Lalamiko hili liibuliwa na walimu wakuu wa Shule za Msingi Burunge, Mwanga, Lake Tanganyika, Mlole na Kahabwa wakati wa zoezi la utoaji elimu mashulenii lilofanywa na Kamtii ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya EWURA CCC mkoa wa Kigoma.

Akiongea kwa masikitiko, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kahabwa Bi. Nuru Kifupi alisema kuwa, shule yake haina huduma ya maji kwa muda wa miezi mitatu baada ya mabomba kukatwa na mkandarasi wa barabara.

Alisema, kutokana na adha hiyo, kila mwanafunzi analazimika kutafuta maji na kupeleka shulenii, jambo ambalo lisingefanyika kama huduma hiyo ingekuwepo na badala yake wanafunzi hao wangetumia muda wao katika kujisomea zaidi ili kuwasaidia katika kupata matokeo mazuri.

"Tatizo la maji linalotokana na uharibifu wa miundombini ya maji kuelekea shulenii kwetu limekuwa ni mwiba kwa wanafunzi wetu kimasomo kwani linahatarisha afya za wana-

funzi na walimu pamoja na kuathiri ratiba za masomo," alieleza Mwl. Kifupi.

Katika kutatua changamoto hiyo, Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Kigoma (RCC) walianza kwa kutoa elimu kwa walimu hao kuhusu umuhimu wa kulalamikia huduma mbovu na kuwashauri kulitumia Baraza katika jitihada zao za kutafuta ufumbuzi wa changamoto kwa kufuata utaratibu mahsusii wa kuwasilisha malalamiko kama ulivyoainishwa kwenye Kanuni za EWURA.

Akielimisha walimu wa shule hizo, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji mkoani Kigoma Bi. Rose Kanango aliwashauri walimu wa shule hizo kutokaa kimya pindi huduma ya maji inapokosekana mashulenii kwani wanaoleteseka ni wanafunzi hivyo watoto taarifa kwa Mamlaka husika ili kupata ufumbuzi.

"Msikae kimya kunapokuwa na ukosefu wa huduma mashulenii, toeni taarifa kwa Mamlaka ya Maji na kama inashindikana leteni lalamiko lenu katika ofisi ya EWURA CCC ili tuwasaidie kufuatilia utatuvi wa lalamiko husika," alisitisiza Bi. Kanango.

Akitoa ufanuzi juu ya malalamiko ya walimu hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma (KUWASA) Mhandisi Jonas Mbike alisema kuwa, hawajopeka malalamiko ya ukosefu wa huduma ya maji kutoka katika shule

hizo lakini aliahidi kufuatilia suala hilo ili kulipatia ufumbuzi.

"Tunawaomba walimu wajenge tabia ya kutoa taarifa wanapokumba na changamoto zinazohusu huduma ya maji, kwani wakikaa kimya sisi pia hatuwezi kujua matatizo yao," alisema Mhandisi Mbike.

Alisema changamoto kubwa inayozikumba shule nyingi kutokua na huduma ya maji ni kuwa na madeni makubwa wanayodaiwa na KUWASA, hivyo kuilazimu KUWASA kusitisha huduma.

"Naomba walimu tushirikiane kuhakikisha huduma za maji mashulenii zinaboreshwala lakini pia iende sambamba na ulipaji wa ankara ili kurahisisha upatikanaji wa huduma husika," alisema Mhandisi Mbike.

Programu za kutembelea shule za msingi katika Manispaa ya Kigoma Ujiji imefanya Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Kigoma kubaini changamoto nyiningi za huduma za maji katika shule hizo. Katika kuhakikisha huduma za maji mashulenii zinaboreshwala, Kamati imejipanga kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha shule hizo zinapatia ufumbuzi wa matatizo yao kwa kushirikiana na mtoa huduma.

Ndugu Benedict Mosha Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati Kigoma akiwa katika eneo la matanki ya maji ya Shule ya msingi Burunge walipotembelea ili kujionea uhaba wa huduma ya maji katika shule hiyo. Picha na Sakina Yusuf



Fahamu utaratibu wa kusitishiwa na kurejeshewa huduma ya umeme

Anadorice Komba na Catherine Charles

Watumiaji wa huduma ya umeme kupitia Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) wanaweza kugawanywa katika makundi mawili kutokana na mfumo wao wa malipo.

a. Wateja wa malipo ya kabla (prepaid customers)

Hawa ni wateja wanaotumia huduma ya umeme kwa kufanya malipo kabla ya huduma. Wateja hawa hulazimika kununua umeme kwa

"uniti" kabla ya matumizi na pindi uniti hizo zikiisha umeme hukatika wenye. Mteja wa kundi hili anaweza kununua umeme kwa kupitia njia mbalimbali za malipo ikiwemo mawakala wa TANESCO, mitandao ya simu, pamoja na benki. Kundi hili lina watumiaji wengi kwa sasa hasa wateja wa majumbani. Mteja wa kundi hili sio rahisi kusitishiwa huduma ya umeme kwa sababu ya kuwa na deni kwa kuwa hawezi kutumia umeme pasipo kuilipia kwanza.

b. Wateja wa malipo ya baada (post-paid customers)

Wateja hawa hufanya malipo baada ya ku-



www.tanesco.co.tz

Tumekuhudumiaje?

Nimeridhika Sana **Nimeridhika** **Wastani**

Sijaridhika **Sijaridhika Kabisa**

Sasa unaweza kutoa mrejesho wa jinsi tulivyokuhudumia kwa kubonyeza link ya tupime.tanesco.co.tz

Tupime au tushauri ili tuendelee kukuhudumia vizuri zaidi.



#Tupokazini

tumia huduma ya umeme ambapo baada ya mteja kutumia huduma hiyo, TANESCO humtumia ankara yake inayooneshwa ni ya mwezi gani, namba ya mita ya mteja husika, darrera ambalo mteja yupo, siku mita il-isomwa, usomaji wa sasa na uliopita, uniti zilizotumika katika mwezi husika na usomaji wa KVA.

Pia ankara hiyo huoneshwa mchanganuo mzima wa ankara ya mteja na jumla ya fedha anazotakiwa kulipa. Pia ankara huambatanishwa namba ya kulipia (control number).

Katika Sheria ya Umeme Sura ya 131, Kanuni za Umeme [The Electricity (Supply Service) Rules] za 2019 zilizochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 387; Kanuni ya 47 (1) TANESCO inawajibika kusoma mita ya mteja wa malipo ya baada ili kuji-ridhisha kiasi cha umeme uliotumika angalau:

- Mara moja ndani ya miezi 6 kwa wateja wakubwa; na
- Mara moja ndani ya miezi mitatu kwa wateja wengine.

Wateja wa umeme wa kundi hili, wanaweza kusitishiwa huduma ya umeme endapo watachelewa au kushindwa kulipa ankara zao kwa wakati. Kulingana na Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO kipengele namba 5 ukurasa wa 8 na 9 kinaelekeza utaratibu ufuato ufuatwe katika kusitisha na kureje-

sha huduma ya umeme kwa wateja:

Usitishaji wa huduma

Kama ilivyo katika sheria ya umeme namba 10 ya mwaka 2008 kifungu cha 28; mwenye leseni ya kutoa huduma ya umeme anawenza kukata umeme kwa mteja ambaye atakiuka wajibu wa kimkataba wa kupatiwa huduma ya umeme mpaka hapo atakapolipa deni lake lote la nyuma pamoja na ada ya kurudishiwa umeme. Kwa hiyo:

a. TANESCO itakata umeme kwa wateja wote wenyewe kukiuka utaratu-bu uliowekwa.

b. Umeme utakatwa siku 7 baada ya muda wa malipo ulioelekezwa kwenye bili ambapo ni sawa na siku 14 baada ya tarehe ya kutolewa bili.

c. Kabla ya TANESCO kukata huduma kwa mteja ni lazima mteja apelekewe taarifa ya kukata umeme kutokana na kushindwa kulipa bili, taarifa hiyo ni ya masaa 48 baada ya siku 14 alizopewa kupita.

d. TANESCO itakata umeme si zaidi ya saa mbili kabla ya muda wa kufunga sehemu za kufanya malipo au vituo vya malipo.

e. Kukata umeme hakutafanyika siku ya mwisho wa wiki au siku za mapumziko ya umma.

f. TANESCO haitoruhusiwa kusitisha huduma ya umeme kwa mteja katika siku za Jumamosi, Jumapili au

siku za mapumziko zinazotabulika kitaifa.

Katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO kifungu (g) ukurasa wa 8 umetoa ruhusa ya kumkatia mteja huduma ya umeme siku yoyote ya wiki endapo mteja atagundulika kuwa anaiba umeme, kwa njia ya kuchezea mita au mfumo wake, kutumia umeme bila kupimwa, kujiunganishia umeme baada ya kukatiwa, ama kujiunganishia njia ya umeme au mita ya umeme isivyo halali.

Mtumiaji hatasitishiwa huduma ya umeme mpaka baada ya saa 48 ya notisi yamefika baada ya siku 14 kupita toka tarehe ambayo mteja alipokea bili yake.

Ikiwa TANESCO itasitisha huduma kwa mteja tofauti na taratibu tajwa hapo juu, basi mtoa huduma atawajibika kurejesha huduma ya umeme mara moja.

Urejeshaji wa huduma baada ya mteja kulipia

Kurudisha umeme kutafanywa mapema iwezekanavyo na siyo zaidi ya siku ya kwanza ya kazi baada ya malipo kamili ya madai ya matumizi, na mteja atalipia ada ya kurudishiwa umeme (reconnection fees) kiasi cha shilingi 8,000/=.

Endapo TANESCO itamkatia umeme mteja kimakosa kwa madai ya kutolipia matumizi, TANESCO itawajibika kumfidia mteja husika kama ilivyooneshwu katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO kifungu cha 5(h).

Kupitia Makala hii ni muhimu kwa watumiaji wa huduma ya umeme kulipia huduma waliyotumia kwa wakati kama moja ya wajibu wao amba ni kulipa ankara kwa wakati na kuondokana na usumbuwa wa kusitishiwa huduma. Ankara isipolipwa kwa wakati itasababisha huduma kutokuwa endelevu.

Ni muhimu watumiaji kutumia huduma ya umeme kwa uhalali na siyo kufanya udanganyifu kwa nia ya kuepuka kulipa bili. Pia wito unatolewa kwa watumiaji wa huduma ya umeme kutoa taarifa kwa mtoa huduma pale wanapogundua mita ina shida au matumizi ya umeme yameshuka au yamepanda ghafla.

“

Umeme utakatwa siku 7 baada ya muda wa malipo ulioelekezwa kwenye bili ambapo ni sawa na siku 14 baada ya tarehe ya kutolewa bili

“

Mtumiaji hatasitishiwa huduma ya umeme mpaka baada ya saa 48 ya notisi yamefika baada ya siku 14 kupita toka tarehe ambayo mteja alipokea bili yake

Uramba wafurahia mita za maji za kielektroniki

Na Sakina Yusuf, Tabora

Wananchi wa kijiji cha Uramba kilichopo katika kata ya Kalunde ndani ya Manispaa ya Tabora wamefurahia mita za kielektroniki ambapo sasa watakuwa na uhakika wa kupata maji kwa saa 24.


Huduma ya majisafi ni moja kati ya huduma muhimu katika maisha ya kila siku ya binadamu na viumbe hai wengine. Hata hivyo, si kila mwananchi anaweza kumudu gharama ya kulipia kuunganisha huduma ya maji kutoka katika mamlaka za maji nchini.

Katika kuhakikisha kila mmoja anapata huduma hii, mamlaka za maji huweka makundi mbalimbali ya watumiaji ikiwemo watumiaji wa maji kupitia 'maghati' au 'kiosk' ili kuwafikia wananchi ambao uwezo wao kifedha ni mdogo.

Watumiaji wamekuwa waki-kumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo kupatikana kwa huduma kwa saa maalum, na wakati mwingine wahudumu kutokuwepo kwenye magati na hivyo kufanya wananchi kukosa huduma ya maji.

Katika kudhibiti changamoto hiyo, Mamlaka ya Majisafi na Usafifi wa Mazingira Tabora (TUWASA) imeamua kufunga mfumo wa mita za maji za kielektroniki ili kuisaidia kutatua changamoto hiyo. Kwa kutumia mita hizo mteja hupokea "sarafu" au "tag" ambayo atatakiwa kuilipia malipo kabla ya matumizi kupitia mitandao ya simu na kwa kuweka tag/sarafu yake kwenye gati la maji ambalo huruhusu maji kutoka mpaka sarafu hiyo itakapondolewa kwenye gati.

Moja kati ya wanufaika wa huduma hii ni wananchi wa kijiji cha Uramba kilichopo katika kata ya Kalunde ndani ya Manispaa ya Tabora ambako EWURA CCC Tabora imeshuhudia teknolojia hiyo walipotembelea Kijiji hicho kuomba nafasi ya kufanya uelimishaji kwa wananchi wa kijiji cha Uramba kuhusu pamoja na mambo mengine masuala yanayohusu huduma za nishati



Asha Hassan mkazi wa kijiji cha Uramba Manispaa ya Tabora, akichota maji kwa kutumia sarafu yake katika moja ya maghati ambayo TUWASA imeyawekea mfumo wa maji wa kielektroniki. Picha na Mpigapicha Wetu

na maji.

Akiongea na EWURA CCC Tabora, Mwenyekiti wa kijiji hicho ndugu Abdallah Shabani Mgusi amesema kuwa, wananchi wamefurahishwa sana kwa huduma hiyo kuwekwa ambapo sasa watakuwa na uhakika wa kupata huduma ya maji kwa saa 24 bila usumbufo wowote kwani mwananchi akiwa na sarafu yake ambayo imelipiwa basi atapata huduma.

"Tunafurahia kwa kweli maji yanapatikana katika ghati kwa saa 24 ukiwa na sarafu yako unapata maji," alisema ndugu Mgusi.

Naye Salma Bakari ambaye pia ni mkazi wa kijiji cha Uramba alisema kuwa kwa sasa hakuna foleni wala usumbufo kutoka kwa wasimamizi kwani anaweza kujipangia muda wa kwenda kuchota maji bila kuwa na hofu ya kutomkuta msimamizi wa ghati, akiweka tu sarafu yake anapata maji.

"Nikiwa na sarafu yangu najipangia mwenyewe muda wa kwenda kuchota maji bila kuwa na hofu ya kukosa huduma," alisema Salma.

Akiongelea kuhusu mfumo huo mpya, Meneja ufundi wa TUWASA Mhandisi Juma Kusekwa alisema kuwa ni kweli TUWASA imeweka mfumo wa maji wa kielektroniki kwenye baadhi ya maghati na mfumo huu umeleta mafanikio makubwa, si tu kwa wateja lakini pia kwa Mamlaka.

Alisema Mamlaka imeweza kusanya mapato kwa uhakika kupitia mfumo huo tofauti na awali ambapo mapato yalikusanywa mkononi na wasimamizi wa maghati hayo.

"Mfumo huu wa maji wa kielektroniki umeisaidia sana Mamlaka kuongeza ukusanyaji wa mapato yake na kudhibiti upotevu wa maji kuto-ka kwa wateja wa maghati ambao awali ilikuwa ni changamoto. Kupitia teknolojia hii tunaweza kusimamia kwa ukaribu zaidi na kujua kila kitu kinachotokea kwenye vituo," aliongea Mhandisi Kusekwa.

Kutokana na faida kubwa zitokanazo na matumizi ya Mita za kielektroniki kwenye sehemu za kiosk, EWURA CCC kupitia Kamati yake ya watumiaji mkoani Tabora inazishauri Mamlaka za Maji katika mikoa mingine kuujaribu mfumo huo ili kupunguza changamoto za huduma ya maji katika maghati ikiwemo changamoto ya upotevu wa maji.

HUDUMA YA UONDOSHAJI MAJITAKA KWA KUTUMIA GARI



**KATIKA KUENDELEA KUBORESHA HUDUMA YA UONDOSHAJI MAJITAKA,
MKURUGENZI MTENDAJI WA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA JIJINI TANGA (TANGA UWASA) ANAWAJULISHA WATEJA NA
WANANCHI WA JIJI LA TANGA KUWA SASA IMEANZA RASMI KUTOA HUDUMA
YA UONDOSHAJI WA MAJITAKA KWA KUTUMIA GARI MAALUMU KWA
GHARAMA NAFUU SANA ZINAZOANZIA TZS 50,000 - 102,000 KULINGANA NA
UMBALI.**

f i t s d e TangaUwasa s 0735800111 c 0800110111Bure.

"Kila Tone Lina Thamani"

WIZARA YA MAJI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)




**Marekebisho ya Miundombinu ya Majitaka
Eneo la Dodoma road Yakiendelea. Usafi wa
Mazingira ni Dhamana Yetu**

t 0800 110 122 i @iruwa.sa f @Irwuasa_Iringa

HabariPicha



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (kushoto) akiielekea kwenye kikao cha majadiliano katika ofisi za TANGA UWASA baada ya kutembelea chanzo cha maji eneo la Mabayani, katikati ni ndugu Gipson George Katibu wa Waziri wa Maji na wa kwanza kulia ni Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC, Tanga Bi. Nuru Zuberi. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Kagera (RCC), ndugu Eustadi Katunzi (aliyesimama katikati) akitoa elimu juu ya huduma za nishati na maji kwa wanafunzi wa shule ya msingi Kashozi iliopo Bukoba vijijin.



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala Mkao wa Kagera bi Anadorice Komba (aliyeshika kipaza sauti) akitoa elimu kuhusu vidokezo vya huduma za nishati na maji kwa wakazi wa mtaa wa Kabanga Milembe kata ya Hamghembe Manispaa ya Bukoba.

HabariPicha



Ndugu Miraji Vanginothi, Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa (RCC) akitoa elimu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wauguzi iliyofanyika Gangilonga katika Manispaa ya Iringa.



Bw. Charles Lwabulala, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Iringa akiwa na Katibu wake Bw. Miraji Vanginothi walipokuwa wakitoa elimu kwa wananchi mkoani Iringa kuitia Radio NURU FM 93.5.



Miraji Vanginothi Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa huduma za nishati na maji Mkoa wa Iringa akitoa elimu kuhusu EWURA CCC na kazi zake kuitia Furaha FM 96.

Makonde boresheni huduma zenu – Baraza

Na Said Ismail, Mtwara

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeishauri Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde kuhakikisha inatoa huduma nzuri kwa watumiaji wa huduma za maji kwenye eneo lao la utoaji huduma ili kuendana na uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya maji unaofanywa na Serikali.

Ushauri huo umetolewa na ndugu Emmanuel Chagu Paul, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWURA CCC Mkoaa wa Mtwara alipokuwa akiwasilisha maoni kwa niaba ya Baraza kufuatia ombi la Mamlaka hiyo kutaka kurekebisha bei za maji kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Akiongea wakati wa uwasilishaji maoni hayo, bwana Paul aliishauri Mamlaka hiyo kutumia fursa ya uwekezaji unaofanywa na Serikali ili kuhakikisha huduma zinakuwa bora na za uhakika ili kupunguza au

kuondoa kabisa malalamiko ya watumiaji wa maji katika eneo hilo.

"Boresheni huduma zenu ili mwananchi anapoomba kuungwa huduma ya maji aweze kuipata kwa wakati unaokubalika na Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), tumieni fursa hii ya ufadhilli mnaouputa kutoka Serikalini kuimarisha na kuboresha huduma," alisitisiza ndugu Paul.

Katika hatua nyingine, wananchi wa Tandahimba na Newala waliohuduria kikao hicho walilalamika kuhusu kutokuwepo kwa huduma ya maji katika maeneo yao na pia kukosekana kwa mahusiano ya kribu kati ya wananchi na Mamlaka ya maji.

"Tatizo hapa siyo bei zinazoombwawa, bali kubwa zaidi ni upatikanaji wa huduma yenye. Unaweza ukaomba kuunganishiwa huduma ya maji na ukakaa Zaidi ya miezi sita bila kupata huduma ilihali umelipia, wakati bomba zimeja madukani," alisema Yusuph Kateule.

Akijibu hoja za wananchi hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde, Mhandisi Francis Bwire alisema wamepokea changamoto zote zilizoainishwa na wananchi na kuwa watazfanyia kazi haraka kadri itakavyowezekana.

"Tumepokea ushauri wote na tutawasiliana na wafanyakazi wenetzu kuhakikisha tumewaunganisha na huduma wateja wote ambaa tayari wamelipia," alisema Mhandisi Bwire.

Naye Bwana George Kabelwa, Afisa kutoka EWURA, akiongea kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa EWURA alisema kuwa, amezipokea hoja zote kwa hatua zaidi na kuongeza kwamba kwa kuwa marekebisho ya bei ni mchakato, basi Mamlaka itakwendwa kuyazingatia maoni yote na kuyafanyia kazi ipasavyo.

"Tumepokea maoni yenu yote na kwenye mchakato huu tutazingatia kila maoni yaliyowasilishwa," alisitisiza Bw. Kabelwa.

EWURA CCC inaendelea kuwawakilisha watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA na kuwasilisha maoni yao kila yanapohitajika ili kutetea haki na maslahi yao huku ikiwakumbusha watumiaji wote kutimiza wajibu wao.



TANGA UWASA

tangauwasa

Facebook

Instagram

YouTube

Twitter

Tovuti

ISO 9001:2015

Tufuatilie katika mitando ya kijamii ili kupata taarifa mbalimbali, Elimu juu ya huduma, kuwasilisha taarifa, malalamiko na maoni juu ya huduma za TANGA UWASA

#hudumakaribuyakozaidi

TUMIA MAJI KWA UANGALIFU, KILA TONE LINA THAMANI!

Piga 0800110111 Bure 0735 800 111 @tangaUWASA

Mpango kabambe wa uelimishaji wawafikia vijana 4,000 Ruvuma

Na Magreth Temba, Ruvuma

Jumla ya wanafunzi 4,014 wa shule za sekondari na msingi Manispaa ya Songea, wamefikiwa na kuelimishwa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA katika kipindi cha Januari hadi Juni 2023.

Idadi hiyo imefikiwa kufuatia mpango kabambe wa uelimishaji mashulenii uliobuniwa na kutekeleza na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya EWURA CCC mkoani Ruvuma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji mkoani Ruvuma ndugu Edmund Mnyawami amesema kuwa, uamuzi wa kuwafikia vijana mashulenii ulifikiwa na Kamati yake baada ya kuona kuwa kuna umuhimu wa kuwajengea uwezo vijana ili wawe sehemu ya wataalamu wa kufundisha makundi rika panapotokea uhitaji huo.

"Vijana ni kundi muhimu katika kuandaa watumiaji wenye uelewa na wenye kutambua nafasi yao kat-

ka kuboresha huduma za nishati na maji nchini. Kama Kamati tumeona kundi hili lisibaki nyuma kutokana na umuhimu wake," aliezea ndugu Mnyawami.

Alisema kwa kushirikiana na wakuu wa shule kwenye Manispaa ya Songea, Kamati ya Watumiaji ya EWURA CCC mkoani Ruvuma itaendelea kutoa elimu kwenye shule mbalimbali ili kuhakikisha elimu kuhusu huduma za nishati na maji zinifikia watu wengi zaidi.

"Tunaelimisha wanafunzi saba-bu nao wanasmama kama mabalozi wetu kwani wanatusaidia pia kufikisha elimu tunayowapa kwa wazazi/walezi wao lakini na wao pia inawapa chachu ya kutekeleza yale waliyojifunza katika kuwa na matumizi mazuri ya huduma za nishati na maji," alisema Mwenyekiti huyo wa Kamati

Alisema Kamati hiyo mkoani humo litaendelea kushirikiana na walimu kila nafasi inapopatikana ili kuwa na wigo mpana wa kuwafikia wanafunzi wengi na kuwaelimisha kuhusu masuala mtambuka kwenye huduma za nishati na maji.

Naye Bi Mariam Kinyunyu, Mwalimu Mkuu katika shule ya Msingi Msamala, alisema kuwa, elimu wanayoipata wanafunzi ni nzuri na inawasaidia katika maisha yao ya kila siku hasa kwenye suala la nishati na maji.

Kwa kweli elimu iliyotolewa ni nzuri sana na imeongeza kitu kipyasi kwa wanafunzi tuu bali hata walimu nasi tumenufaika kwani yaliyo mengi kuhusu mambo ya nishati na maji tulikuwa hatuyafahamu kabisa. Nimependa mada ya matumizi sahihi ya huduma ya maji kwani itasaidia sana wanafunzi kuwa na matumizi mazuri wawapo hapa shullenii na kutupunguzia adha ya kulipa ankara kubwa ya maji," alisema Bi Kinyunyu.

Kamati ya watumiaji mkoani Ruvuma itaendelea kushirikiana na walimu ili kutoa elimu kwa watumiaji wengi zaidi pamoja na kulitangaza Baraza na kazi zake na kuhamasisha umma kushiriki kikamilifu katika kulalamikia huduma mbovu ili kuwa na huduma bora na endelevu inayokidhi uhitaji wa watumiaji.

Uelimishaji



**WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI
WA MAZINCIRIA IRINGA (IRUWASA)**




KUMBUKA

**Kila Kiumbe Kinahitaji Maji. Tulinde Vyanzo na Miundombinu ya Maji.
"Kila Tone Lina Thamani"**

0800 110 122 | @iruwa.sa | @Iruwasa_Iringa

Huu hapa ndio muda mahsus i wa kujaza mafuta katika vyombo vya moto

Na Emmanuel Chagu Paul, Mtwara

Bidhaa zitokanazo na petroli ni muhimu sana katika Buchumi endelevu wa mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Ikiwa bidhaa hizi zitakuwa bora na kupatikana kwa urahisi, kunawenza kuleta matokeo chanya katika uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Mathalan, mitambo mingi ya viwandani pamoja na vyombo vya usafirishaji kama vile magari, pipipiki n.k. vinahitaji nishati ya mafuta ili kufanya kazi.

Miaka ya hivi karibuni, biashara ya usafirishaji kwa njia ya pipipiki maarufu kama 'bodaboda' imeendelea kukua kwa kasi katika maeneo ya mijini na vijijini na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya mafuta kwa vyombo hivi.

Utafiti mdogo kupitia semina za uelimishaji kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa mafuta kama vile madereva wa bodaboda na teksi umebaini kuwa, wengi wao hawajui njia sahihi za kuokoa na kulinda thamani ya pesa zao wanaponunua mafuta kwa ajili ya vyombo vya.

Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu kupata ujazo pungufu wa mafuta mionganoni mwa madereva wa vyombo vya moto. Aidha Mamlaka husika ikiwemo Wakala wa Vipimo wamechukua hatua mbalimbali za kufuatilia na kuchunguza vipimo lakini majibu yalibainisha vipimo kuwa sahihi.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kupertia makala hii linalenga kuelimisha watumiaji wa vyombo vya moto juu ya faida za kujaza au kununua mafuta usiku au asubuhi sana pindi ardhi ikiwa imepoa. Kwa mujibu wa kitabu cha "Ramark Sengupta (May 2014) Petrol, Dizel: Why you Should Refuel in the Morning" kinaleze kuwa, muda mzuri wa kujaza au kununua mafuta ni asubuhi sana kipindi ardhi ikiwa bado na ubaridi. Aidha makala hii inatoa ufanuzi kuhusu wakati sahihi wa kujaza/kutojaza au kununua mafuta ya chombo chako.

a) Usiku

Usiku ardhi hupo na kuwa na ubaridi, hivyo kwa tabia ya mafuta

kipindi cha ubaridi hayatengenezi gesi hivyo husinyaa na kubaki na uhalisia wa ujazo wake. Katika kipindi hiki ukinunua au kujaza mafuta utapata kipimo kilicho sahihi kabisa.

b) Asubuhi

Ukinunua mafuta kipindi cha asubuhi, mafuta chini ya ardhi huwa yana tabia ya kupoa na hutulia na kubaki na uhalisia wa ujazo wake hivyo utapata kipimo kilicho sahihi kabisa.

c) Mchana

Wakati wa jua kali mafuta hubadili tabia kutokana na hali ya joto. Kutokana na joto hilo, mafuta hutanuka na kutengeneza gesi au kuongeza hali ya mvuke hivyo hali hii huathiri mgandamizo na kusbabisha mwenye chombo kutopata kipimo kilicho sahihi. Uzoefu unaoesha kwamba wasafirishaji wengi wa teksi na bodaboda hupenda kujaza mafuta pindi wanapopata mteja. Ujazaji mafuta kwa njia hii unaweza usiwe bora kwani hujikuta wanapatia vipimo visivyo sahihi na pungufu kutokana na jua kali ambalo husababisha hali au umbo la mafuta kutokuwa katika uhalisia wa mgandamizo wake.

EWURA CCC inawashauri madereva wote wa vyombo vya moto kujaza mafuta asubuhi au usiku ili waweze kupata vipimo sahihi.



Bajaji inayotumika kufanya biashara ya usafirishaji abiria ikijaza mafuta muda wa mchana. Picha na Mpigapicha Wetu



Afisa Msaidizi Utawala na Huduma kwa Wateja, EWURA CCC Mkoa wa Geita Ndg. Wadi Omari alipotembelea ujenzi wa mitambo ya kusafisha maji GEUWASA mwezi Juni 2023. Ujenzi huo utakapokamilika utasaidia, pamoja na mambo mengine, kudhibiti kwa kiasi kikubwa maji yanayopotea. Picha na Mpigapicha Wetu

GEUWASA yashauriwa kudhibiti maji yanayopotea

Na Mwandishi wetu, Geita

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita (GEUWASA) imeshauriwa kuongeza udhibiti wa upotevu wa maji kutoka kwango cha asilimia 31 hadi kufikia asilimia 20 kina-chokubalika, kwa kuwa upotevu huo huwaongeza mzigo wa gharama watumiaji kupitia bei za maji.

Ushauri huo umetolewa na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoani Geita (RCC) wakati wa semina ya uelimishaji kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Geita (District Consultative Council-DCC) kilichofanyika Geita.

Akiwasilisha mada ya namna nzuri ya matumizi ya maji, Afisa Msaidizi wa Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWURA CCC ndugu Wadi Omari alisema kuwa GEUWASA ina jukumu la kutoa huduma za majisafi na salama na kuhakikisha

inakuwa na mikakati madhubuti na endelevu ya kudhibiti kiasi cha maji yanayopotea isizidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa.

Aidha Afisa huyo aliendelea kueleza kwamba, GEUWASA inat-akiwa kudhibiti maji yanayopotea ili kuuza maji mengi zaidi ambayo yatakuwa yanawafikia watumiaji wa mwisho na kukusanya fedha za kutosha kutokana na mauzo hayo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa GEUWASA Mhandisi Frank Changawa alisema kuwa, GEUWASA inajitahidi kuhudumia miundombinu yake ya maji na pale inapotokea bomba limepasuka na kupata taarifa, basi muda huo huo hutuma mafundi wake kwenda kushughulikia bomba husika.

Alisema, GEUWASA imepanga mafundi kwenye kila upande wa mji katika kanda saba, na kila upande una fundi ambaye anasimamia miundombinu ya maji.

Akiongea kwenye mkutano huo Mwenyekiti wa Kamati ya

Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Geita Ndugu Dotto Paul alisema kuwa, kazi mahususi ya Kamati ni kuwatetea na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji ikiwemo kuhakikisha Kamati kwa niaba ya Baraza inapaza sauti kuhusu madhara ya upotevu wa kiwango kikubwa cha maji.

"Tunawaelimisha watumiaji watambue madhara ya upotevu wa maji. Tunawafahamisha kuwa, kwango cha maji yanayopotea kutokana na wizi, mivujo au njia nyininge yoyote kinahesabiwa na kujumuishwa kwenye bili zinazotozwa na Mamla-ka. Hivyo tunawahamasisha kutoa taarifa za mivujo na wizi kwa GEUWASA ili nao wawe sehemu ya kudhibiti upotevu huo," alieleza ndugu Paul.

Alisema Kamati pia ina wajibu wa kuwakumbusha watoa huduma juu ya kutekeleza majukumu yao kama vile kudhibiti mivujo ya maji na hivyo kuiomba GEUWASA kuongeza jitihada za kuondoa kabisa changamoto hii katika mji huo.

EWURA CCC mkoani Geita imeendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji ikiwemo kutoa taarifa muhimu zinazohusu maslahi ya watumiaji wa huduma hizo kila zinapopatikana.



Zijue sababu za umeme wa LUKU kuisha haraka na suluhisho lake

Na Amani Mbogo, Dodoma

Moja ya kazi inayofanywa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) ni kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji, ambapo moja ya lalamiko kubwa ambalo huwa linalalamiwa na wananchi baada ya kupata elimu hii ni umeme wa LUKU kuisha kwa haraka.

Mmoja ya watumiaji wa huduma ya umeme, Bwana William Richard, mkazi wa Mtaa wa Hazina, ni mmoja wa wahanga wa lalamiko hili ambapo mwanzoni alikuwa akinunua units 28 za umeme ambazo alikuwa anazitumia kwa muda wa siku 21, ila kwa sasa units hizo huisha chini ya siku 10.

Makala hii inakusudia kukuangazia mambo yanayoweza kusababisha

umeme wa LUKU kuisha haraka pamoja na suluhisho lake.

1) Kuwepo kwa umeme unaovu-ja

Tatizo la umeme kuvuja linaweza kusababisha matumizi ya umeme kuwa makubwa. Watumiaji wengi wa umeme huwa wanajua maji pekee ndiyo yanayouju, lakini umeme pia huvuja hivyo kusababisha units za umeme kuisha haraka na hili mara nyingi linaweza kusababishwa na mkandarasi aliyetumika kuweka mfumo wa umeme asiwe mwenye sifa inayotakiwa au muda mwininge unawezu ukakuta panya amehusika kwenye kuharibuu nyaya za umeme.

2) Kutumia vifaa vya nyumbani vyenye kasoro

Vifaa vya majumbani kama vikitumika vikiwa vina kasoro, ni lazima matumizi ya umeme yatakuwa ni

makubwa. Mfano wa vifaa hivi ni kama pressure na rice cooker, heater ya kuchemshia maji na kadhalika.

3) Kutumia vifaa vingi vya umeme kwa wakati mmoja

Hii ni moja ya sababu inayowezza kufanya matumizi ya umeme kwa mtumiaji yakawa ni makubwa. Watumiaji huwa tuna kasumba ya kutumia vifaa vingi vya umeme kwa wakati mmoja bila kujua, kwa mfano unakuta mtumiaji amewasha feni, muda huo huo amewasha jiko la umeme na pia anayoosha nguo zake, hapa ni lazima mtumiaji atakuja kulalamika kuwa umeme unaisha haraka.

4) Kutumia vifaa vya umeme vya teknolojia ya zamani

Kama mtumiaji bado atakuwa anaendelea kutumia taa za zamani basi matumizi ya umeme ni lazima yatakuwa yanaendelea kuongezeka bila kujua. Taa hizi hutumia umeme mwingu sana.

Suluhisho la umeme wa LUKU kuisha haraka

1. Tumia wakandarasi waliosajiliwa na EWURA katika kuungiza mfumo wa umeme ndani ya nyumba yako ili kuwa na uhakiwa wa usalama wa mfumo wa umeme na njia hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuepukana na tatizo la umeme kuvuja.

2. Mteja ahakikishe anakagua mfumo wa umeme wa nyumbani kwake ndani muda wa miaka mitano.

3. Epuka kutumia vifaa vya umeme vyenye kasoro (faulty) sababu vifaa hivi vinatumia umeme mwingu sana.

4. Unashauriwa kutumia taa za 'energy saver' kwani zimeonesha uwezo wa kukabiliana na matumizi makubwa ya umeme.

5. Unashauriwa kutumia vifaa vipyaa vya umeme na kuepuka vifaa vya teknolojia ya zamani, sababu vifaa vya teknolojia ya sasa vimetengenezwa kwa ajili ya kumpuza matumizi makubwa ya umeme.

EWURA CCC Mara yabuni mbinu mpya utoaji elimu kwa wananchi

Na Dennis Ndanu, Mara

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuitia Kamati yake ya Watumiaji Mkao wa Mara imebuni mbinu mpya ya kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma hizo kwa kuafuata katika maeneo yao mbalimbali ya mikusanyiko.

Robinson Wangaso, Mwenyekiti wa kamati ya watumiaji Mkao wa Mara amesema kamati hiyo imeanzisha utaratibu wa kuweka Hema (GAZEBO) eneo la Bustani ya Malkia Elizabeth wa Uingereza lilopo katikati ya mji wa musoma ambapo wananchi wanafika kupumzika katika bustani hiyo wanapata elimu ya matumizi sahihi ya huduma, haki na wajibu wa mtumiaji pamoja na njia sahihi ya kuwasilisha malalamiko pindi watumiaji hao wanapokabiliana na changamoto au kero kutoka kwa watoa huduma za nishati na maji.

Wangaso alisema baada ya Ka-

mati yake kutoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwemo akina mama wajasiriamali kuitia vikundi nya kijamii, vijana kutoka Madhehebu ya Dini za Kristo na Misikiti, wawakilishi wa asasi za kiraia, waendesha pikipiki (Bodaboda), Walimu Wakuu wa shule za msingi, sekondari na vyuo, akina mama wa majumbani, watu wenye ulemavu, viongozi wa serikali za mitaa, Madiwani na makundi mengine, sasa wameamua pia kuafuata wananchi katika maeneo ya mikusanyiko na masoko.

"Tulianza utaratibu wa kufanya uhamashishaji na utoaji elimu katika mikusanyiko ya masoko ya Nyamatare, Nyakato kwa saa Nane, Nyasho na kituo cha mabasi Bweri, sasa tumeamua kuhamishia ofisi yetu katika viwanja nya bustani ya Malkia Elizabeth ambayo watu wengi wanafika kupumzika na pia kutembelea hema letu la EWURA CCC kwa lengo la kupata elimu ya matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji," alisema Wangaso.

Mwenyekiti huyo alisema mbinu

hiyo imewezesha kufikia watumiaji wengi ambapo kwa siku moja watumiaji kati ya 20 hadi 30 wamekuwa wakifika katika banda na kujipatia vipeperushi, maelezo na ufanuzi kutoka kwa wajumbe wa kamati ambapo hutoa elimu hiyo kwa zamu na kuwa itaendelea kutumika kutokana na kuonesha mafanikio makubwa ya kuafikia watumiaji wengi kwa gharma nafuu.

Kwa upande wake Neema Chacha ambaye ni moja ya watu walitembelea hema la EWURA CCC na kupata elimu alisema kuwa, awali alikuwa hajui mambo mengi juu ya haki na wajibu wa watumiaji wa huduma za maji na nishati lakini baada ya kutembelea hema ameweza kupata elimu na kujua haki zake nyingi kama mtumiaji wa huduma za maji na nishati.

"Kwa kweli mnatuelimisha mambo mengi, vitu vingi hatukuwa tunajua wala kuwa na elimu navyo, kumbe nina haki nyingi ambazo nimezipoteza na kuzipuzia, nashukuru sana EWURA CCC kwani mnaleta mwanga kwa sisi wananchi" alisema Neema.

Neema aliahidi kuwashihii wananchi wenzake kutembelea hema na ofisi za EWURA CCC mijini Musoma ili nao waweze kupata elimu juu ya huduma za Nishati na maji kwa manufaa yao katika Maisha yao ya kila siku.

Uelimishaji

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI
MAMILAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI BABATI - BAWASA**



S.L.P 245, MIYOMBONI, BABATI MANYARA, SIMU NA. 027-2510004 BARUA PEPE: info@bawasa.or.tz TOVUTI: www.bawasa.or.tz



DIRA YETU

Dira yetu ni kuwa Mamlaka bora ya mfano kwa kutoa huduma bora za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini Tanzania

DHIMA YETU

Dhima ya Mamlaka ni kutoa huduma bora za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Babati kwa kutumia taalamu, na teknolojia rafiki kwa mazingira

MIONGOZO NA SHERIA

- > sheria ya maji Na.12 ya mwaka 2009.
- > Mkataba wa makubaliano na taratibu za uendeshaji kati ya BAWASA, Wizara ya Maji na Umwagiliaji na EWURA

HISTORIA FUPI

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA) ni Taasisi ya Serikali yenye jukumu la kutoa huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Babati. BAWASA ipo daraja "C". Taasisi hii ilianzishwa rasmi tarehe 13/12/2002 kufuatana na sheria Na. 8 ya mwaka 1997 na marekebisho ya liofanyika kwa sheria ya maji Na.12 ya mwaka 2009.



"MAJI NI UHAI"

"KILA TONE LINA THAMANI KUBWA"

HUDUMA KWA WATEJA


WASILIANA NASI KUPITIA NAMBA ZIFUATAZO:

- . 0677 025537
- . 0677 025538

PIA TEMBELEA FACE BOOK PAGE YETU

<https://web.facebook.com/bawasa2004>

MALIPO YA BILI

 <p>1. NMB BANK 2. NMB MOBILE 3. NMB WAKALA</p>	 <p>NAMBA YA KAMPUNI 100200</p>	<p>MALIPO YA BILI PEKEE</p>
---	--	------------------------------------

 <p>1. TIGO PESA PEKEE</p>	 <p>NAMBA YA KAMPUNI 200416</p>	<p>MALIPO YA BILI PEKEE</p>
--	--	------------------------------------







'Toeni elimu kuhusu usomaji dira za maji'

Na Wadi Omari, Geita

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita (GEUWASA) — imehimizwa kutoa elimu ya kutosha kwa watumiaji kuhusu usomaji wa dira (mita) za maji na namna zinavyofanya kazi ili kuondoa malalamiko ya ankara zisizo sahihi.

Wito huo umetolewa na ndugu Khalfan Msemo, Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Geita wakati wa mkutano wa wadau wa GEUWASA uliofanyika mjini Geita ambapo GEUWASA iliwasilisha maombi na kusanya maoni ya wadau wake kuhusu dhamira ya kufanya marekebisho ya bei ya maji.

Akielezea umuhimu wa GEUWASA kutoa elimu sahihi juu ya usomaji wa dira za maji, Ndugu Msemo alisema kuwa, GEUWASA inapaswa kuhakikisha kuwa inatoa elimu ya kutosha kwa wateja wake juu ya usomaji wa dira za maji na jinsi ya kukokotoa ankara za wateja hao.

"Kama GEUWASA itaelimisha wateja wake namna ya kusoma dira za maji, hiyo itakuwa ni hatua muhimu katika utatuzi wa changamoto ya malalamiko yanayowasilishwa kuhusu ankara kubwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa GEUWASA Mhandisi Frank Changawa alisema GEUWASA imejipanga kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wateja wake na kwamba hakuna sababu ya kumbambikia mteja wake ankara ambayo

hajaitumia.

Mhandisi Changawa alisema kuwa, elimu ya usomaji wa mita ni muhimu kwa kila mtumiaji wa huduma ya maji yanayotolewa na GEUWASA, kwani hicho ndio kipimo pekee kinachotumika kwa wateja kuitambua kiasi cha maji alichotumia na kupata gharama halisi ya matumizi yake kwa uniti moja aliyoitumia.

Mahitaji ya maji kwa wananchi wa Geita ni makubwa sana, na ifahamike kuwa huduma hii ya maji haina mbadala na hivyo kila wakati binadamu akihitaji maji anatakiwa kupata huduma hiyo na si vinginevyo. Hivyo, uelewa wa usomaji wa dira za maji utasaidia kuongeza uelewa miongooni mwa watumiaji wa huduma hiyo ili kuepuka migogoro na malalamiko yasiyo ya lazima.

Afidiwa kwa kukatiwa maji kimakosa

Na Nuru Zuberi, Shinyanga

Mkazi wa Mtaa wa Mlepa, kata ya Ndala mkoani wa Shinyanga Ndugu Rajabu Masatu Bwire amefidiwa kiasi cha shillingi laki moja na elfu hamsini baada ya kukatiwa huduma ya maji kimakosa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA).

Fidia hiyo imetolewa baada ya EWURA CCC Mkao wa Shinyanga kutoa elimu kwa wananchi juu ya haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwenye mkutano uliofanyika kata ya Ndala, mtaa wa Mlepa mnamo tarehe 23.3.2023.

Akitoa ushuhuda wake wakati wa mkutano huo, ndugu Bwire amesema EWURA CCC kuititia elimu iliyoitoa imemsaidia yeze kujua haki na wajibu wake kama mtumiaji wa huduma za nishati na maji na hivyo kumwezesha kuwasilisha lalamikio lake kwa msaada wa EWURA CCC na hatimaye kulip-

wa fidia.

"Sambamba na elimu niliyopata, Baraza limekuwa nami bega kwa bega katika kuhakikisha napata haki yangu ya msingi," aliezea ndugu Bwire.

Akizungumzia lalamiko lake, ndugu Bwire alisema kuwa, SHUWASA ilimkatia huduma ya maji lakini baada ya kufuatilia iligundulika kuwa wakati anaunganishiwa huduma ya maji dira yake ilifungwa kimakosa kwa mteja mwингine na hivyo kuonekana ana deni ambalo lilimpelekea kusitishiwa huduma ya maji.

"SHUWASA imekuwa ikinzungusha mara kadhaa na baada ya kufuatilia sana ndipo ikagundulika kuwa diraa yangu imefungwa kwa mtu mwингine," alisema ndugu Bwire na kuongeza kuwa aliamua kutafuta msaada EWURA CCC ambapo ilimsadia kupeleka lalamikio lake SHUWASA na ikakubali kumfidia kiasi cha shillingi laki moja na elfu hamsini baada ya kuamriwa kwenye kikao cha usuluhishi.

Aidha aliishukuru EWURA CCC kwa msaada wake kuititia elimu ya

haki na wajibu wa mtumiaji kwa kumpa mwanga wa wapi pa kuanzia huku akitoa wito kwa Baraza kuendelea kutoa elimu zaidi kwa jamii.

Kwa upande wake Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) kuititia Meneja Biashara ndugu Reuben Mwandumbya, ilikiri kutokea kwa changamoto hiyo ya ndugu Bwire kupewa mita ya mteja mwингine na pia kumkatia maji kimakosa na kwamba SHUWASA iliridhia kuititia kikao cha usuluhishi kumlipa mteja kiasi cha shilingi 150,000/=.

"Ni kweli kwamba ilitokea changamoto hiyo kwa mteja ambapo fundi wetu alichanganya dira ya maji lakini tumefanikiwa kumaliza changamoto hiyo na mteja wetu kwa kumlipa fidia," aliezea ndugu Mwandumbya.

EWURA CCC mkao wa Shinyanga itaendelea kutekeleza majukumu yake likiwemo jukumu la kuwasidia wateja wa huduma za nishati na maji kupata haki zao kwa kuwaelimisha kuhusu njia sahihi ya kupata haki hizo.



Huu hapa umuhimu wa mabango ya bei za mafuta kwa watumiaji

Na Catherine Ochido na Anadorice Komba

Mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ni bidhaa muhimu sana kwa watumiaji wa huduma hii. Kipindi cha hivi karibuni maeneo mengi ya mjini na sasa hata maeneo ya vijijini tunaona ujenzi wa vituo vya mafuta na hii yote inaonesha ni kwa kiasi gani watumiaji wa vyombo vya moto wanavyoongezeka siku hadi siku.

Kwa mujibu wa kanuni za mafuta za 2022, tangazo la serikari namba 150 kanuni ya 45 (1) inavitaka vituo vyote vya mafuta kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango (billboard) yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara (promosheen) zinazotolewa na kituo husika.

Bei za mafuta ambayo yanauzwa katika kituo cha mafuta zinat-akiwa kuonekana katika bango na ziwe katika thamani ya shilingi na si vinginevyo, hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 45 (3) ya kanuni za mafuta nchini.

Kanuni hizo zimeenda mbali zaidi, kwani kanuni ya 45 (4) inaonesha aina ya bango lazima liwe la neonni au liwe linaloonesha ujumbe wa bei ukipita katika bango (electronic massage) na bei hizo zioneckane vizuri ili watumiaji wanapokaribia katika

bango la kituo kwa umbali angalau mita hamsini walione vizuri na kwa uwazi.

Katika Makala hii waandishi wanalenga kuonesha umuhimu wa kuwepo kwa mabango haya ya bei kwenye vituo nya mafuta, ambapo swali lifuatalo litakuwa na majibu sahihi:

Je, kuna umuhimu wa kuwepo kwa mabango ya bei katika vituo vya mafuta?

Ndio, upo umuhimu mkubwa kwa vituo vya mafuta kuonyesha bei za mafuta kutokana na sababu zifatazo;

i Ufahamu wa bei elekezi ya mafuta

Kituo cha mafuta kinapoonesha bei ya mafuta katika mwezi husika, inasaidia mtumiaji kutambua bei elekezi ya mafuta ya eneo hilo kwa mwezi husika, mfano, lita moja ya mafuta ya petrol kwa mwezi Juni, 2023 kwa eneo la Bukoba mjini ni shilingi 3,089, dizeli shilingi 2,878 na mafuta ya taa shilingi 3,044 kwa lita, ila kama kuna punguzo lolote la bei basi mtumiaji atawezekuona kupitia mabango hayo.

ii Haki ya kuchagua

Watumiaji wa huduma za mafuta (Petroli, dizeli na mafuta ya taa) kupitia bei katika mabango ambayo

Moja ya kituo cha mafuta kilichopo Bukoba mjini kikiwa na bango ambalo linaonesha bei elekezi za mafuta. Picha na Catherine Ochido

yamewekwa na watoa huduma, yanatoa nafasi kwa watumiaji kuchagua ni kituo gani aweke mafuta kutokana na ulinganifu wa bei kwa wakati husika lakini pasinkuwa na bango linaloonesha bei ingekuwa vigumu sana mtumiaji kuchagua wapi akaweke mafuta. Wateja wana-shauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani.

iii Kutambua aina ya mafuta yaliyopo katika kituo cha mafuta

Kituo cha mafuta kinapoonesha bei ya mafuta pia huonesha aina ya mafuta yaliyopo katika kituo husika na kama mafuta hayo hayapo basi hayataonekana katika tangazo la bei na hii inasaidia watumiaji kutambua mafuta ambayo hayapo katika kituo hicho ili waweze kwenda katika kituo kingine kupata huduma hiyo.

EWURA CCC inawashauri wamili wa vituo kuhakikisha wanakuwa na mabango yanayoonesha bei kwa sababu ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja.

Pia watumiaji wasisite kutoa tarifa pale vituo vya mafuta vinaposhindwa kuonesha bei au kuwauzia mafuta kwa bei tofauti na iliyoelekeza na mamlaka na ambayo haipo katika mabango yao. Watumiaji pia wanaweza kuangalia bei kikomo ya bidhaa za mafuta ya petrol na dizeli kwa eneo husika kupitia simu zao za mkononi kwa kupiga *152*00# na kisha kufuata maelekezo.

HabariPicha



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvvi Mh. David Silinde, akisikiliza maelezo ya kazi za Baraza kutoka kwa Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja Bi Sakina Yusuf alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yaliyofanyika mkoani Tabora mwishoni mwa mwezi Mei, 2023. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja Bi Sakina Yusuf akitoa elimu ya mtumiaji kwa mwananchi aliyetembelea Banda la EWURA CCC wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Maziwa mwezi Juni, 2023.



Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati zinazodhibitiwa na EWURA mkao wa Tabora Ndugu Alfred Pigangoma (wa kwanza kulia) akitoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA kupitia kipindi cha pambazuko kinachorushwa na radio Uhai Fm. Wengine ni MwenyeKITI wa Kamati ya Watumiaji Mkao wa Tabora Bi Catherine Mgaya (katikati) na mtangazaji wa Radio Uhai Bi Diana KataBarwa.

HabariPicha



*Bi. Noela Ntiluvakule, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA
CCC Mkoa wa Pwani akielimisha wakazi wa Mtaa wa Kilimahewa, Wilaya ya Kibaha
kuhusu haki na wajibu wa Mtumiaji wa huduma za Maji na Nishati.*



*Ndugu Saidi Kabirigi, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma
za Maji na Nishati Mkoa wa Pwani, akitoa elimu kuhusu uwasilishaji wa
malalamiko kwa watoa huduma kwa wanafunzi wa shule ya Msingi.*



*Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala mkoa wa Pwani Bi. Noela
Ntiluvakule akiwaelimisha wanafunzi wa shule ya sekondari ya wasichana
Kibaha juu ya Baraza na kazi zake wakati wa programu ya utoaji elimu kuhusu
Baraza na kazi zake kwa wanafunzi wa sekondari.*



Upanuzi wa Miundombinu ya Majisafi Eneo la Mkoga-Manispaa ya Iringa Ukiwa Unaendelea

📞 0800 110 122 📱 @iruwa.sa 📡 @Irufasa Iringa

Aina sita za wateja wa huduma za maji

Na Noela Ntiluvakule, Pwani

Maji ni hitaji la msingi na haki kwa binadamu wote pamoja na viumbe hai, ni muhimu kwa maisha na mazingira, pia ni rasilimali muhimu sana katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Rasilimali ya Maji hugusa nyanja zote za kiuchumi na kijamii kwani hutumika kwa ajili ya shughuli za majumbani, kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, wanyamapori, uzalishajinishati ya umeme, michezo na burudani. Pamoja na shughuli nyingine nyingi.

Kumekuwa na malalamiko kwa watumiaji kuhusu kupatiwa bili kubwa za matumizi ya maji na wakati mwininge wateja wa matumizi ya kawaida kujikuta wanapokea Ankara kubwa kama zile za wateja wa wenye viwanda.

Kwa kuzingatia umuhimu wa maji kwa maisha ya watu, EWURA CCC Mkoa wa Pwani ilitembelea ofi-

si za DAWASA - Kibaha ili kuweza kufahamu aina za wateja wake na namna walivyowagawa kutokana na matumizi yao.

Ndugu Alpha Ambokile, Meneja wa DAWASA Kibaha alitoa ufanuzi juu ya anina za wateja wao, "Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) tumewagawa wateja wetu katika makundi mbalimbali kama ilivyo katika mkataba wa wetu wa huduma kwa wateja wa Julai 2020".

Ambokile alisema mteja wa DAWASA ni mtu ye yeyote aliyeunganishwa kwenye miundombinu ya DAWASA na kupata huduma ya Majisafi na uondoaji wa majitaka. Wateja wa DAWASA wamegawayika katika makundi yapatayo sita kulingana na matumizi yao kama yanavyobainishwa hapo chini:

1. Wateja wa majumbani: Hawa ni wateja wanaotumia maji kwa matumizi ya kawaida ya nyumbani kama kupika, kuosha vyombo, kufua na kadhalika.

2. Wateja wa Taasisi: Hawa ni taasisi zote za serikali, zisizo za serikali na mashirika mbalimbali. (shule, hospitali, vituo vya huduma za Afya, Vyuo Vikuu, Magereza, Polisi na Nyumba za ibada)

3. Wateja wa matumizi ya kibashara: (Hoteli, Maduka, Nyumba za kulala wageni, Migahawa na Vilabu)

4. Wateja wanaotumia maji kwa matumizi ya viwanda.

5. Maghati ya kuuzia maji (Kioksi)

6. Waosha magari

Aidha Ambokile alifanua kuwa katika makundi hayo, gharama za matumizi ya majitaka kwa wateja wenye huduma ya majisafi itatozwa kwa asilimia 80 ya majisafi yaliyotumiwa. Gharama ya majitaka itatozwa VAT asilimia 18, hivyo gharama ya majitaka itakuwa shilingi 455.48 kwa mita ya ujazo. Gharama ya EWURA itakuwa asilimia 1 ya gharama zote zilizotajwa hapo juu. Makundi haya hayana tofauti kwenye gharama ya uniti moja ya kulipa Ankara.

SHUWASA yaipongeza EWURA CCC

Na Joseph Ndataala na Nuru Zuberi, Shinyanga

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) imelipongeza Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuititia Kamati yake ya Mkoa wa Shinyanga kwa kuwa mionganoni mwa wadau waliochangia SHUWASA kushika nafasi ya kwanza katika tuzo za mwaka 2021/2022 zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa kupunguza upotevu wa maji kwa mwaka.

Pongezi hizo zimetolewa na aliyejekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA Mhandisi Yusuph Katopola wakati wa kikao na wadau kili-choitishwa na SHUWASA kwa lengo la kuwashukuru wadau mbao wamekuwa wakitoa taarifa mbalimbali zikiwemo za mivujo ya maji zilizowezesha SHUWASA kudhibiti upotevu na kuibuka Mamlaka bora katika udhibiti wa upotevu wa maji kwa mwaka 2021/22 kati ya mamlaka 26

za mikoa Tanzania Bara, ushindi uliopatia Mamlaka hiyo tuzo.

“EWURA CCC ni mionganoni mwa wadau wakuu wa SHUWASA waliochangia upatikanaji wa tuzo hii kwani wamekuwa wakitupatia taarifa muhimu ikiwemo upotevu wa maji kwenye maeneo tofauti tofauti katika Manispaa ya Shinyanga,” alisema Mhandisi Katopola.

Ikiwa ni ishara ya shukrani na kutambua mchango wake kwa SHUWASA, Mhandisi Katopola alimkabidhi bwana Joseph Ndataala, Mjumbe wa

Ndugu Joseph Ndataala (kulia, Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Shinyanga akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga, Mhandisi Yusuph Katopola wakati wa hafla ya utoaji zawadi kwa wadau wa SHUWASA. Katikati ni Nsianeli Gerald, Afisa Uhusiano SHUWASA. Picha na Mpigapicha Wetu

Kamati ya Watumiaji ya Mkoa wa Shinyanga zawadi za miamvuli pamoja na shajara zenyenembo ya Mamla-ka hiyo.

“Tunaomba mpokee zawadi hizi kama ishara ya shukrani zetu na kutambua mchango wenu kwa taasisi yetu,” alisema Katopola wakati wa ku-kabidhi tuzo hiyo.

Naye ndugu Joseph Ndataala kwa niaba ya EWURA CCC, aliishukuru SHUWASA kwa zawadi hizo na kwa kutambua mchango wake katika utoaji wa taarifa na kusema kuwa, EWURA CCC imekuwa ikishirikiana na SHUWASA kutatua changamoto za uvujaji wa maji kwenye kila eneo linaloonekana kuwa na mvujo na kupewa ushirikiano wa haraka na wafanyakazi wa Mamlaka hiyo kila walipotoa taarifa.

“Ahsanteni sana kwa zawadi hizi na tunaipongeza SHUWASA kwa kuwa wasikiuu kwani mmekuwa mkitoa ushirikiano wa kutosha na kwa haraka tunapowapa taarifa za mivujo,” alisema Ndataala.

EWURA CCC Shinyanga imekuwa ikiwaelimisha wakazi wa Manispaa ya Shinyanga na vitongoji vyake kutoa taarifa kwa mto wa huduma au kwenye ofisi za Baraza zilizomo mkoani huo kila kunapokuwa na changamoto ya maji ikiwemo mivujo.



Baraza lashuhudia uzinduzi Mradi wa Maji Makongo, Bagamoyo



Mheshimiwa
Waziri Mkuu
Kassim Majaliwa
(MB) akiutubia
wananchi wakati
wa uzinduzi wa
Mradi wa Ujenzi
wa Mfumo wa
usambazaji maji
kati ya Makongo na
Mji wa Bagamoyo
uliofanyika katika
viwanja vya shule
ya msingi Tegeta
A, jijini Dar es
Salaam. Picha
Noela Ntiluvakule

Na Noela Ntiluvakule, Pwani

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoja wa Pwani limeshiriki katika hafla ya uzinduzi wa Mradi wa Ujenzi wa Mfumo wa Usambazaji Maji kati ya eneo la Makongo na Mji wa Bagamoyo uliofanyika Machi 16, 2023 katika viwanja vya shule ya msingi Tegeta A, jijini Dar es Salaam.

Shughuli ya uzinduzi huo ilihudhuriwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa mgeni rasmi na ndiye aliyezindua Mradi huo ulioambatana na maadhishimo ya Wiki ya Maji kwa mwaka 2023.

Katika hotuba yake Mhe. Waziri Mkuu Majaliwa alilitaka Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na wa-

Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuhakikisha inawaunganishia huduma ya Maji wananchi wote waishio katika eneo la mradi, na kusitiza kuwa, watumiaji wa huduma za maji wasikubali kutoa rushwa ya aina yoyote ili kupata huduma hiyo.

“Ni msisitizo wa Wizara ya Maji na Serikali, hakuna rushwa yoyote utakayoitao kwa kuunganisha maji kuja nyumbani kwako, uunganishwaji ni wa gharama zile zile.”

Aidha alilitaka mamlaka zote za maji nchini kutokutoza watumiaji ankara kubwa za maji kinyume na matumizi yao na kila mwananchi atakayewekewa mita aelimishwe namna mita hiyo inavyofanya kazi ili kusiwe na malalamiko.

Alihitimisha kwa kuzitaka Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na wa-

nanchi wote kuhakikisha wanaturza na kuhifadhi vyanzo vya Maji.

Mhe. Waziri Mkuu alisisitiza kwa kusema “Pamoja na jitihada zote hizi zinazofanywa kupeleka Maji kwa wananchi kama vyanzo vyetu haviko salama wala tusitegemee kupata maji, suala la kupata maji ni la sisi wenye.”

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso ambapo katika hotuba yake alieleza kuwa, mradi huo umelenga kuwaletea nafuu ya Huduma za Maji Watumiaji katika Wilaya ya Kinondoni katika kata za Changanyikeni, Vikawe, Goba, Mivumoni, Mbweni, Madale, Tegeta A, Bunju, Wazo, Ocean Bay na Salasala. Kwa upande wa Bagamoyo mradi huo utahudumia watumiaji wa kata za Mataya, Sanzale, Migude, Ukuni, Mtambani, Nianjema,

Kimara ngo'mbe, Kisutu na Block 'P'.

Waziri alieleza kwamba pamoja na uzinduzi wa mradi huo wa maji bado wapo wananchi ambao hawaajaungani shiwa huduma ya maji, hiyo alimuagiza Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Bw. Kiula Kingu ahakikishe kuwa wananchi wote walioomba maji waunganishiwe ndani ya siku saba kama Mkataba wa Huduma kwa Wateja unavyosema.

Aweso aliyasema hayo baada ya kubaini kuwa kuna baadhi ya maeneo, wananchi wanataka huduma ya maji na wanakaa miezi mitatu na zaidi pasipo kuunganishiwa na huduma hiyo.

Waziri Aweso aliongeza kuwa, "Ni haki kwa mwananchi kupatiwa huduma ya maji na mwananchi ana wajibu wa kulipia ankara za maji lakini hatutakubali kuona msoma mita anambambikia mwanaanchi ankara ya maji."

Pia aliwaomba wananchi kutokaa kimya bali walalamikie kila sehemu wanayonna wanapata changamoto na kuahidi kuwa, kwa yejote atakayebainika kukwamisha huduma za maji safi na salama hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Katika uzinduzi huo mambob mbalimbali yanayohusu haki za watumiaji yalijadiliwa kuanzia muda wa kuunganishiwa huduma, changamoto wanazokutana nazo baadhi ya watumiaji ikiwemo vitendo vya kuombwa rushwa, ankara kubwa za maji na ukosekana-ji wa vifaa hasa mita za maji, yote hayo Mhe. Aweso aliatolea ufanuzi kwa manufaa ya watumiaji wote nchini.

EWURA CCC Mkoa wa Pwani itaendelea kuhakikisha inalinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za Nishati na Maji kwa kutoa tarifa muhimu za watumiaji.

Apunguziwa deni hadi shilingi 6,300

Na Nuru Zuberi, Tanga

Baraaza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na maji (EWURA CCC) mkoa wa Tanga limemsaidia Mzee Shaabani Kissena mkazi wa Mwam-boni Tanga kutatta changamoto yake ya ankara kubwa ya maji ya shilingi 188,000/= kutoka Tanga UWASA am-bayo kiuhalsia haikuwa ikiendana na matumizi ya mteja huyo.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya mzee Kissena kufika kwenye ofisi za EWURA CCC Tanga mapema mwezi Machi, 2023 kwa lengo la kutoa lalamiko lake juu ya changamoto yake hiyo.

Akieleza kuhusu lalamiko la ndugu Kissena, Afisa wa Ankara na Makusanyo wa Tanga UWASA ndugu Daudi Mkumbo alikiri kupokea lalamiko la namna hiyo na kusema kuwa lilitokana na changamoto kwenye upande wa mfumo wa uchakataji wa ankara na hiyo kusababisha Mzee Kissena kupata ankara isiyo na uhalsia.

"Tunashukuru kwa kufuatilia lalamiko la mteja na nikiri kwamba tumepeata changamoto kwenye mfumo wetu wa ankara," alisema Mkumbo na kuongeza kuwa Mamlaka imere-

kebisha deni la mteja huyo kutoka Tsh.188,000/= hadi tsh. 6,373.37 am-bayo ni bili halisi ya mteja.

Kwa upande wake Kissena alii-shukuru EWURA CCC kwa kumsaidia kupunguziwa ankara ya maji na kuhidi kuwa balozi mzuri kwa wengine wenye uhitaji kama yeye kwa kuwashauri watembelee ofisi za EWURA CCC kwa msaada zaidi.

"Ninashukuru sana ofisi ya EWURA CCC na sasa nimeridhika na ankara hii ya Tsh.6,373.37 kwani hiyo ndio inaendana na matumizi yangu halisi," alisema Kissena.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoani Tanga ndugu Andrew Nkusi aliujezea mpango wa Baraza wa kuendelea kupaza sauti kwa kutoa elimu kwa watumiaji ili wachukue hatua stahiki katika kushughulikia kero zinazohusiana na huduma za nishati na maji na kufuatilia kwa ukaribu malalamiko ya wateja yanapojitokeza.

"EWURA CCC kuititia Kamati yake ya watumiaji mkoani Tanga itazidi kuwfuatilia kwa ukaribu wadau wake ili kuhakikisha wanaridhika na huduma zinazodhibitiwa na EWURA," alisema ndugu Nkusi.

Baraza lashauri suluju ujazo wa LPG

Na Mwandishi wetu, Mbeya

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na maji ya EWURA CCC mkoani Mbeya, imeishauri Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuona umuhimu wa kufanya marekebisho ya Kanuni zinazosimamia utoaji wa huduma ya gesi ya kupikia majumbani (LPG) ili kutoa fursa kwa wasambazaji wakubwa wa gesi hiyo kuwapatia mizani ya kupima uzito wa mitungi wauzaji wa rejareja ili kuondo changamoto ya malalamiko dhidi ya uzito pungufu wa bidhaa hiyo.

Akiongea wakati wa mkutano ulioitishwa na Wakala wa Vipimo (WMA) mkoani Mbeya, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWAURA CCC Bi Mwasiti Athumani alisema kuwa, suluju ya malalamiko ya uuzwaji wa ujazo pungufu wa gesi kwenye mitungi itapatikana kama Mdhibiti atafanya marejeo ya Kanuni ili kuruhusu wasambazaji wakubwa wa kampuni za gesi kuwapatia wauzaji wadogo mizani ya kupimia mitungi ya gesi wanayouza.

Kwa upande wao wauzaji wadogo walilalamikia faida ndogo wanayopata kwenye mitungi ya gesi ukilinganisha na bei za mizani ya kuning'iniza ambayo imepitishwa kupima gesi huku wakidai kuwa, mizani ya aina hiyo huuzwa kwa takriban laki mbili huku mizani wa kidigitali ukiuzwa kuanzia laki nane.

"Mara nyingi baada ya bei elekezi za gesi kutoka, faida ya mitungi huwa haizidi 2,000/= kwa mitungi mikubwa na 1,500/= kwa mdogo, sasa kwa faida hii utaweza kununua kweli mizani?"

Kama msambazaji mkubwa atawawezesha wauzaji wadogo wadogo kwa kuwapa mizani, atakuwa amewasaidia sana wauzaji hao jambo ambalo ni faida kwa msambazaji mkubwa kwani muuzaji mdogo atauza mitungi ya gesi kutoka kwa kampuni moja pekee



mdogo, sasa kwa faida hii utaweza kununua kweli mizani?" alihoji Bw. Adam Solomon, mfanyakiasa mizani, atakuwa amewasaidia sana wauzaji hao jambo ambalo ni faida kwa msambazaji mkubwa kwani kwa kufanya hivyo muuzaji mdogo atauza mitungi ya gesi kutoka kwa kampuni moja pekee jambo ambalo pia ni takwa la kikanuni kuwa mitungi ya aina tofauti isichanganywe sehemu moja ili kuepuka madhara ikiwemo milipuko.

Aliishauri WMA kuona umuhimu wa kuwawezesha kwa kuwakopesha wauzaji wadogo mizani ya kupimia kwa makubaliano ya kurejesha kidogo kidogo kwa kuwa WMA ndio mamlaka iliyopewa dhamana kusimamia vipimo kwa niaba ya Serikali.

Kwa upande wake Meneja Masoko kutoka kampuni ya ORYX Bw. Idan Mushi alisema kuwa, kampuni ya ORYX inasikiliza maelekezo ya Mdhibiti juu ya nini kifanyike na kwamba wapo tayari kupokea maelekezo ili kulinda haki na maslahi ya watumiaji pamoja na kuboresha utoaji wa huduma zao.

Naye Bwana Raphael Nyawamu, mwakilishi kutoka EWURA na Bw. Kajungu, Meneja wa Mkoa WMA walikiri kupokea ushauri na maojni hayo na kusema watayafikisha kwenye ngazi za juu za taasisi zao hoja hizo kwa ajili ya kujadiliwa ili waone kama itafaa kufanya mabadiliko hayo na kupunguza malalamiko na changamoto juu ya uzito/ujazo wa bidhaa za gesi za kupikia majumbani.

Wakala wa Vipimo (WMA) iliishisha kikao hicho kilichohusisha wauzaji wadogo wa gesi, mawakala wa usambazaji gesi mkoani wa Mbeya, waandishi wa habari pamoja na wadau kutoka sekta ndogo ya nishati ya gesi kwa lengo la kukusanya maoni juu ya nini kifanyike ili kupunguza au kuondo kabisa malalamiko kutoka kwa watumiaji wa gesi za kupikia majumbani kuhusu uuzwaji wa uzito pungufu wa mitungi ya gesi ya kupikia majumbani.



EWURA CCC yashiriki ziara ya Waziri wa Maji Tanga

Na Mwandishi wetu, Tanga

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za nishati na Maji (EWURA CCC) limeshiriki kwenye ziara ya Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso Mbunge wa Pangani iliyofanyika mwezi Januari, 2023 kwa lengo la kujionea hali ya hupatikanaji wa huduma ya maji mkoani Tanga.

Waziri Mhe. Aweso amefanya ziara hiyo kufuatia kuwe po kwa changamoto ya ukose fu wa huduma ya maji Jiji ni Tanga kwa kipindi cha zaidi ya siku mbili na hivyo kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kujitokeza katika jiji hilo.

Kupitia ziara hiyo ya Waziri, Baraza lilipata mwaliko kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira TANGA UWASA wa kushiriki kwa kuitambua mchango wake katika masuala mbalimbali yanayohusu huduma ya maji.

Mbali na EWURA CCC ziara hiyo ya Mhe. Aweso ilihuisha pia ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tanga, uongozi wa Chama na Serikali ngazi ya wilaya ya Tanga mjini pamoja na wameshimiwa Madiwani wa kata

mbalimbali za Jiji la Tanga.

Katika ziara hiyo, Waziri Aweso pamoja na viongozi wengine mbalimbali walitembelea chanzo cha maji cha Mabayani, mitambo ya kuzalisha, kusafisha na kutibu maji iliyopo eneo la Mowe.

Kupitia ziara hiyo, Waziri alibaini kuwa changamoto ya ukosefu wa huduma ya maji katika jiji la Tanga ilisababishwa na chanzo cha uzalishaji maji cha TANGA UWASA ambacho kilizidiwa na tope na hivyo kuifanya Mamlaka hiyo kusitisha uzalisha wa maji.

Akifanya majumuisho ya ziara hiyo, Waziri Aweso alisema "Tumefika hadi kwenye chanzo cha maji na kujionea, maji yamekuwa na tope jingi sana, maana yake ni kwamba, chanzo kikuu cha maji katika jiji la Tanga ni Mto Zigi, yawezekana katika mto huo kuna shughuli kubwa za kibinadamu zinafanyika, kwa hiyo shughuli za kibinadamu zinapofanyika zinasababisha kuharibu chanzo cha maji."

Katika ziara hiyo, Mhe. Waziri na viongozi hao walitembelea baadhi ya nyumba za wananchi zilizounganishiwa huduma za maji katika eneo la Chumbageni na Ngamiani Kaskazini ili kujionea hali hal-

isi ya upatikanaji wa huduma ya maji.

Mhe. Aweso alijiridhisha kuwa hali ya huduma imerejea na inaendelea kuimarika hatua kwa hatua katika maeneo mbalimbali ikiwemo pembezoni mwa Jiji.

"Tumejjridhisha kwa kwenda baadhi ya nyumba kwa mfano nyumba ya kwanza Chumbageni Maji yamerudi kwenye hali yake," alisema Waziri Aweso.

Akihitimisha ziara hiyo, Waziri Aweso aliwahimiza watendaji wa TANGA UWASA kutengeneza utaratibu wa kutoa taarifa kwa wananchi pin-di panapotokea changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji ili kuepusha Malalamiko kutoka kwa watumiaji wa huduma hiyo, lakini pia pawepo na utaratibu wa kushirikishi viongozi wa Serikali za Mitaa kwa kuwa kwakufanya hivyo itarahisisha kufikisha tarifa sahihi kwa wananchi.

EWURA CCC Mkoo wa Tanga katika kutekeleza Majikumu yake, imekuwa ikishirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali na hivyo kujenga mahusiano mazuri ya kikazi yanayosababisha kuwepo na ushirikiano kati ya Baraza na taasisi hizo.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (MB - katikati) akikagua mabwawa ya kusafisha maji Mowe, kulia ni Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Bi. Nuru Zuberi na washiriki wengine kwenye ziara hiyo. Picha na Mpigapicha Wetu



Yajue makosa, adhabu kwenye huduma ya maji

Na Chipegawai Samwel, Morogoro

Sheria namba 5 ya maji ya mwaka 2019 imeanisha makosa yanayoweza kutokea kwenye huduma ya maji pamoja na adhabu zake. Adhabu zilizoanishwa kwenye Sheria ya Maji zinaweza kujumuishwa na adhabu zilizoainishwa kwenye sheria ya makosa ya jinai pamoja na sheria

ya makosa ya uhujumu uchumi wa nchi. Yafuatayo ni makosa pamoja na adhabu zake: -

1. Kutumia maji vibaya (kifungu na. 63)

Mtu ye yeyote anayetumia maji vibaya au kuruhusu/kusababisha maji kutumiwa vibaya mfanano kuyachezea au kutoyatumia kwenye mambo ya msingi anatenda

kosa. Ingawaje ni kosa ambalo linione kana halifuutiliwi sana ila faini yake ni shilingi laki tano na isiyozidi milioni kumi au kifungo cha miezi sita jela mpaka miaka miwili au vyote viwili.

2. Kuharibu miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira (Kifungu na. 61)

Mtu ye yeyote anayevuruga au

kuharibu mfumo mzima wa huduma ya maji, miundombinu kama mita, mabomba, viungio, mabwawa, mitambo pamoja na vipuli au kuingilia kazi za majisafi na usafi wa mazingira atakuwa anatenda kosa ambapo faini yake ni kiasi cha shilingi laki tano lakini siyo zaidi ya shilingi milioni 50 au kifungo cha muda usiopungua miaka mitano gerezani au vyote viwili kwa pamoja.

Kulingana na sheria ya uhujumu uchumi wa Tanzania, kuchezea miundombinu ya Serikali faini au adhabu ya kosa hilo litaangaliwa na uzito wake.

3. Kuchepusha maji kutoka kwenye laini (Kifungu na. 62)

Hii inamaanisha kutopitisha maji kwenye mita ili yasihesabive au kuchepusha toka kwenye chanzo cha maji au pampu, kujiunganishia huduma ya maji pasipo kufuata utaratibu wa kisheria uliowekwa. Faini ya kosa hili ni kuanzia kiasi kisichopungua shilingi laki tano hadi milioni hamsini au kifungo cha kisichopungua miezi kumi na mbili mpaka miaka mitano jela au vyote viwili kwa pamoja.



Mtu yeyote

anayetumia maji yanayotolewa na mamlaka husika kwa madhumuni mengine isipokuwa yale ambayo aliomba atakuwa anatenda kosa. Mfano badala ya matumizi ya majumbani, mtumiaji anaamua kuuza maji, umwagiliaji wa shamba, lisilo bustani.

4. Kuchezea dira za maji au kuharibu (Kifungu na. 64)

Mtu yeyote anayebadilisha au kusababisha au kuepusha dira isipime kipimo sahihi (isizunguke, kuigeza au kuizua isifanye kazi inayostahili) kwa lengo la kupata usambazaji mkubwa wa maji kuhiko ule anaostahili au kukwepa malipo ya usambazaji maji atakuwa anatenda kosa ambapo faini yake ni shilingi laki tano mpaka milioni kumi au kifungo kisichopungua miezi sita mpaka miaka miwili jela.

5. Kutumia maji kinyume na matumizi uliyoomba (Kifungu na. 65)

Mtu yeyote anayetumia maji yanayotolewa na mamlaka husika kwa madhumuni mengine isipokuwa yale ambayo aliomba atakuwa anatenda kosa. Mfano badala ya matumizi ya majumbani, mtumiaji anaamua kuuza maji, umwagiliaji wa shamba, lisilo bustani. Faini ya kosa huili ni kiasi cha shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi sita (6) jela. Bila kuathiri hakiki ya mamlaka ya maji, adhabu hii itaangalia kurejesha thamani ya maji yaliyotumika vibaya.

6. Kuoga kwenye miundombinu ya maji (Kifungu na.66)

Mtu yeyote ambaye;

- Anaoga au kuogesha kwenye chanzo au eneo la maji au miundombinu inayotumika na mamlaka ya maji;
- Anaosha au kutupa/kuruhusu kutupa mnyama, nguo, nyenzo au kitu chochote kwenye chanzo au miundombinu inayotumika na mamlaka ya maji;
- Anafunga au kufunga chanzo cha maji au miundombinu ya maji;

Atawajibika kulipa faini ya kiasi cha shilingi elfu hamsini mpaka milioni moja au kifungo cha muda usiopungua mwezi mmoja mpaka mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

7. Kuchafua/Uchafuzi wa maji kwenye chanzo (Kifungu na. 67)

Mtu yeyote ambaye;

- Anayeweka au kuruhusu nyenzo yoyote ardhini au kimiminika kinachoweza kusombwa/

kubebwa kuelekea kwenye eneo la chanzo cha maji au mitambo ya maji atatozwa faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni moja mpaka milioni tano au kifungo cha miezi kumi na mbili mpaka miaka mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

• Kama nyenzo au kimiminika kimesombwa na kuingia kwenye majisafi na usafi wa mazingira atatozwa faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

• Atainua au kujenga au kusababishwa kujengwa kwa muundo wowote wa muda au wa kudumu na kusababisha hitilafu/tobo kwenye sehemu yoyote ya miundombinu ya maji atawajibika kulipa faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni moja mpaka milioni kumi na kifungo cha miezi sita mpaka miaka miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

8. Kutupa taka ambazo hazi-jaaishwa (Kifungu na 68)

Mtu hatakiwi kutupa au kusababishwa kutupwa kwa taka yoyote ambayo haijaidhinishwa kwenye usafi wa mazingira. Anayekiuka jambo hili atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni moja na isiyozidi milioni tatu au kifungo cha miezi sita hadi miaka miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

9. Kuwazuia maafisa wa maji kufanya kazi yao/kumpiga au kumtolea lugha chafu

Wakati wa utekelezaji wa wajibu wao, kama mteja ana wasiwasi na afisa wa mamlaka ya maji husika, basi amuombe kitambulisho, au apige simu kwa mamlaka ya maji husika kujiridhisha au kutoa taarifa. Kumzuia afisa wa Mamlaka asifanye kazi yake, kumpiga au kumtolea lugha chafu ni kutenda kosa ambapo faini yake ni kiasi cha shilingi milioni mbili na haitazidi milioni tano na kifungo cha miaka mitatu jela.

Watumiaji wa huduma ya maji wanashauriwa kufuata sheria, karnuni na taratibu ili kuepuka makosa ambayo yameanishwa kwenye sheria ya maji.

HabariPicha



Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiai wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mhandisi David Ngula (wa pili kushoto) akieleza malengo ya Baraza kutembelea MORUWASA mbele ya vyombo vya habari wakati wa ziara ya Baraza kutembelea Mamlaka hiyo. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Morogoro (MORUWASA) Mhandisi Tamim Katakweba akieleza namna MORUWASA inavyofanya jitihada za kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Mkao wa Manyara Neema Nniko akifanua jambo kwenye kikao cha utoaji mrejesho wa marekebisho ya bei za maji kilichoitishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA) mwezi Mei, 2023

HabariPicha



Bi Neema Nnko Afisa Msaидизи Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Mkoa wa Manyara, akileleza jambo aliposhiriki kikao cha wananchi wa kata ya Mwada kilichofanyika hivi karibuni. Katika kikao hicho, Baraza lilitoa elimu na usafanuzi kuhusu haki na wajibu kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji.



Afisa Msaидизи Huduma kwa Wateja na Utawala, EWURA CCC mkoa wa Manyara Bi Neema Nnko akitoa elimu kwa wananchi wa Kijiji cha Halla wakati wa mukutano wa wananchi ulioandalishi na Serikali ya Kijiji.



Afisa Msaидизи Huduma kwa Wateja na Utawala mkoa wa Pwani Bi.Noela Ntiluvakule akiwaelimisha wanafunzi wa shule ya sekondari ya wasichana Kibaha juu ya Baraza na kazi zake wakati programu utoaji elimu kuhusu Baraza na kazizake kwa wanafunzi wa sekondari.

Baraza laombwa kuendelea kutoa elimu Mkataba Huduma kwa Mteja

Na mwandishi wetu, Dodoma

Waandishi wa habari wa radio Uzima wameliomba Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mkoa wa Dodoma kuongeza nguvu katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Mkataba wa huduma kwa mteja.

Akiongea wakati wa uelemishaji kwa njia ya radio hiyo mwezi Mei, 2023, mwandishi wa habari wa kituo hicho cha radio ndugu Soud Captain alisema kuwa, mkataba wa huduma kwa mteja ni muhimu kwani utamfanya mtumiaji wa huduma za nishati na maji kujua utaratibu wa kushughulikiwa malalamiko yake pindi anapopata changamoto katika huduma hizo.

"Kwa upande wangu ninaomba EWURA CCC muendelee kuwekeza nguvu katika kutoa elimu juu ya mkataba wa huduma kwa mteja. Leo tumepata elimu muhimu sana pamoja na wasikilizaji wetu. Mathalani mimi binafsi sikuwa nafahamu kuwa Mkataba wa Huduma za Maji unapaswa uzingatие Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji za Mwaka 2020, Chapisho (GN) No. 849, Kanuni ya inayolekeza kwamba huduma ya maji inapaswa iunganishwe

kwa mteja mpya ndani ya siku saba za kazi baada ya kulipia ghamama za maunganisho mapya na kwamba siku hizo zikipita mteja ana haki ya kudai na kulipwa fidia," alieleza Captain.

Naye mwandishi wa habari Bi Avelina Mussa alisema kuwa ofisi ya EWURA CCC ni vyema ihakikisha kuwa watoa huduma wanaheshima na kutekeleza yaliyomo kwenye mikataba hii ili watumiaji waweze kupata huduma za nishati na maji kwa wakati husika.

"Kwanza niwapongeze sana EWURA CCC kwa hatua nzuri na kazi mnayoifanya ya kuhakikisha mnawafikia wananchi wengi sana kwa kutumia vyombo vya habari ikiwemo radio yetu ya Uzima ili waweze kujua umuhimu wa mkataba wa huduma kwa wateja, leo tumejifunza kuwa Mkataba wa huduma kwa wateja wa huduma za umeme na maji unatoa haki kwa mteja kupewa taarifa kuhusu katizo la huduma hasa ambalo limepangwa tofauti na lile la dharura na pia unataja muda maalum wa katizo hilo, hata hivyo, watoa huduma ni mara chache sana wanafanya hivyo kwa mfano kwenye umeme mkataba unasema taarifa yoyote ya katizo ambalo limepangwa litatolewa ndani ya siku 10 kabla ya katizo lenyewe lakini mara nyin-

gi unaweza kupata taarifa ndani ya siku moja" alisema Bi Mussa.

Akiwajibu waandishi hao, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWURA CCC (Dodoma) Bwana Amani Mbogo aliahidi kuwa Baraza litaendelea kutumia vyombo vya habari pamoja na mikutano ya hadhara kuhakikisha elimu juu ya mikataba ya huduma kwa wateja inawafikia wananchi wengi.

"Kama mlivyosema, mikataba hii ni muhimu sana kwa wananchi wetu. Ofisi yetu inaendelea kutumia vyombo vya habari vya hapa mkoani kwetu ikiwemo Radio Uzima pamoja na mikutano ya hadhara ya wananchi ili kuhakikisha tunawafikia wananchi wengi zaidi. Pia tutaendelea kukumbusha watoa huduma wakiwemo DUWASA na TANESCO kuwa ni muhimu kuwapatia wateja wao mikataba hii wakati wowote, hususan i wakati wanapounaganishwa na huduma zao ili kujenga uelewa wa wateja hao na kuepuka malalamiko yasiyo ya lazima," alisema Bw. Mbogo.

Ofisi ya EWURA CCC Dodoma itaendelea kutoa elimu kwa watumiaji wengi zaidi kuhusu kazi za Baraza kwa ujumla na pia kuhakikisha kero mbalimbali za watumiaji zinafutiliwa na kupatiwa ufumbuzi kwa wakati.



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala, EWURA CCC Dodoma, Amani Mbogo (kulia), akielimisha umma kuhusu masuala yanayohusu watumiaji wa huduma za nishati na maji kupitia kituo cha Radio cha Uzima. Picha na Mpigapicha Wetu



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja EWURA CCC Mkoa wa Mara ndugu Dennis Ndanu (kulia) akimfanulia jambo mwananchi aliyetembelea banda la EWURA CCC wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika kweneviwanja vya Shule ya Msingi Mukendo Manispaa ya Musoma mwaka 2023. Picha na Mpigapicha Wetu

Wiki ya Sheria yawanufaisha wakazi Manispaa Musoma

Na Dennis Ndau, Mara

Watumiaji wa huduma za nishati na maji nchini wametumia maadhi-misho ya Wiki ya She-ria nchini kutoa na kufikisha mala-miko na changamoto zinazowakabili kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWU-RRA CCC) kupitia Kamati yake ya mkoa wa Mara.

Katika ushiriki wake kwenye maadhimisho ya Wiki ya Sheria, Kamati ilipokea jumla ya malalamiko na maswali 102 kutoka kwa wananchi ambao ni watumiaji wa huduma za nishati na maji ambapo mionganini mwake, 45 yalihusu changamoto za bei za mafuta, 32 yalihusu huduma za maji na 25 yalelekezwa kwa sektanidogo ya umeme.

Wananchi hao walifika katika madhimisho ya Wiki ya Sheria nchini ambayo katika Mkoa wa Mara yalifa-

nyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Mukendo kuanzia tarehe 23 Januari hadi tarehe 1 Februari 2023 siku ambayo ilikuwa ni kilele cha maadhimisho havyo.

Miongoni mwa malalamiko/mas-wali yaliyopokelewa ni kutoka kwan-dugu Rhobi Chacha Mtatiro, mkazi wa Nyarusurya Manispaa ya Musoma aliyealamika kuhusu bei za kuungan-ishiwa umeme na kushauri kuwa, bei hiso zizingatie hali halisi ya maisha yan-wananchi bila kubagua eneo analoishi.

Ndugu Mtatiro alidai kwamba kwenye maeneo ya mjini wapo watu wenye maisha duni sawa na vijijini hivyo ghamama za kuunganishiwa umeme ambazo shilingi 27,000/= kwa wananchi wenye maisha duni vijijini pia zitumike kwa wateja wenye maisha kama hayo waishio mijini.

"Tupo wananchi wenyewe uwezo
mdogo wa kifedha lakini tunaishi
mjini na tumejenga nyumba zetu kwa

gharama ndogo kwa kudunduliza, tunahitaji huduma ya umeme lakini tunashindwa kutohana na gharama za hadi shilingi 320,000 kiwango ambacho ni cha juu mno kwa watu wenye kipato duni kama chetu, alieleza ndugu Mtatiro.

Alisema kuwa, umeme ni hudu-ma muhimu inayopaswa kila mtu ai-pate tena kwa gharama nafuu maana mtumiaji analipia huduma hiyo kilaa anapoitumia, tena ikiwezekana wa-tumiaji waunganishiwe umeme hata-bila malipo ya awali, na gharama za malipo hayo zilipwe kidogo kidogo kuitia manunuzi ya umeme.

Akitoa ufanuzi kuhusu gharama za kuunganishiwa umeme, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Mara Mhanda-si David Chisoti alisema kuwa, kwa mujibu wa Kanuni na taratibu zilizopo sasa, wateja wanaounganishiwa umeme kwa bei ya Shilingi 27,000/= ni wale wa vijijini pekee na siyo mijini.

"TANESCO inatekeleza maagizo na sheria zilizopo na kwamba kwasasa gharama za maunganisho ni shilingi 27,000/= kwa wateja wa vijijiini na 320,000 kwa wanaohitajihuduma wakiwa mjini," alifafanua Mhandisi Chisoti.

Kuhusu katizo la umeme bila tarifa, Mhandisi Chisoti alisema kuwa TANESCO hutumia njia mbalimbali kutoa taarifa ya katizo la huduma ikiwa ni pamoja na magari ya matangazo, barua, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kufikisha taarifa muhimu kwa jamii ikiwa kuna makatizo yaliyopangwa kwa muda fulani. Hata hivyo, Chisoti alikiri kuwepo kwa changamoto mbalimbalii ikiwa ni pamoja na makatizo ya dharura ya umeme ambayo hutokea bila kupangwa au kukusudiwa am-bayo huwa hayatolewi taarifa mape-ma kwa wananchi.

Nae Kaimu Mkurugenzi wa Mam-laka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) ndugu Etropia Pius Ndowo alikiri kuwepo kwa chan-gamoto kadhaa kuhusu upatikanaji wa huduma ya maji hususani uhaba wa vifaa kwa ajili ya maunganisho mapya.

Ndugu Ndowo alisema kuwa, kumekuwa na ongezeko la maombi mapya ya kuunganishiwa huduma ya maji kutokana na kukamilika kwa miundombinu ya mradi wa BALIMA

Ingaendelea Ukk. 38

Fahamu utaratibu wa kulipa bili ya maji

Na Neema Nnko, Manyara

Matumizi bora ya maji na ulipaji wa akara kwa wakati ni jambo muhimu kwa watumiaji kuendelea kupata huduma bora kutoka kwa mto huduma.

Pamoja na elimu inayotolewa na Mamlaka za Maji kuhusu utaratibu wa kulipia bili, watumiaji wengi hawafahamu utaratibu huo wa kulipa ankara ikiwa ni pamoja na kujua ni ndani ya

muda gani anapaswa kulipa ankara yake baada ya kuipoea. Makala hii itaeleza kwa ufupi kuhusu utaratibu wa kulipa ankara yako ya maji ili kuepuwa usumbufu wa kusitishiwa huduma.

Je baada ya mteja wa huduma ya maji kupokea ankara anapaswa kulipa ndani ya muda gani?

Kwa mujibu wa Kanuni ya 51(1) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira 2020, Tangazo



la Serikali Na 849 imeeleza kuwa mteja atatakiwa kulipa bili yake ndani ya siku 30 kutokea pale alipo-pokea bili yake, na kama hatakuwa na uwezo katika kipindi hicho, Kanuni ya 51(2) inampa fursa ya kufanya mazungumzo ya namna atakavyo-bili hiyo.

Katika kipindi hicho, mteja huyo ataendelea kupata huduma kama kawaida. Kwa mujibu wa Kanuni 51 (3) mto huduma anaweza kusisha huduma ya maji wakati wowote endapo siku thelathini zitakwisha bila ya bili kulipwa na kama hakutakuwepo na mawasiliano yoyote kati ya mteja na mto huduma.

Pia sasa unaweza kufahamu deni lako la maji na kupata namba ya malipo (control number) kuitia simu yako ya mkononi ili kufanya malipo kwa urahisi.

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya EWURA CCC Mkoa wa Manyara imekuwa ikitoa elimu kwa watumiaji wa huduma za maji, mionganoni mwake ikiwa ni kuhusu wajibu wa watumiaji kulipa ankara zao za maji kwa wakati ili kuepusha usumbufu wa kusitishiwa huduma pamoja na kuiwezesha Mamlaka ya Maji husika kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi. Kamati itaendelea kutoa elimu zaidi kwa watumiaji ili wafahamu namna ya kuendelea kupata huduma bora kwa kutimiza wajibu wao.

Wiki ya Sheria yawanufaisha wakazi Manispaa Musoma

ambao unapeleka maji katika kata za pembezoni mwa Manispaa ya Musoma zikiwemo Buhare, Kigera, Kwangwa, Bweri na baadhi ya kata za halmashauri wa Wilaya ya Butiama. Ongezeko hili limepelekeea upungufu wa vifaa kukidhi maombi hayo mapya ya wateja.

Aidha Ndowo alisema pamoja na ongezeko hilo la malalamiko, MUWASA imejipanga kuhakikisha wahitaji wote wa huduma wanaunganishiwa ndani ya muda unaokubalika licha ya kuwa uwezo wa Mamlaka kwa kipindi hiki ni asimilia 95 ya maombi ambayo yameweza kufanyiwa kazi kwa wakati.

"Tumejipanga kwa sasa kuhakikisha tunawaunganisha wateja wetu wote walioomba huduma ya maji kwani sasa tuna vifaa nya kutosha,"

alisema Ndowo.

Katika kuadhimisha wiki hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Mara walitumia fursa hiyo pia kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji kuhusu matumizi sahihi ya huduma, kanuni za ubora wa huduma za maji na usafi wa mazingira, videkezo muhimu kwa watumiaji wa huduma za bidhaa za petroli na huduma nyingine.

Robinson Wangaso, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Mara aliwaeleza wananchi walitembelea banda la Baraza kwenye maonesho hayo kuwa EWURA CCC inao wajibu na jukumu la kutetea haki na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA ikiwemo kupokea na kusambaza

taarifa muhimu zinazohusu huduma na bidhaa hizo. Moja ya dhamira ya Baraza ni kutetea watumiaji na kuzaza ufahamu kwa umma kuhusu haki na wajibu wao, kuendeleza uhusiano mzuri wa kazi kati yake na wadau mbalimbali wakiwemo watoa huduma, kuwaleta pamoja watumiaji wa huduma, kushirikiana na mtandao wa watunga sera, vyombo nya habari, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na makundi mbalimbali ya kijamii.

EWURA CCC Mara itaendelea kuelimisha wadau kuitia majukwaa mbalimbali ikiwemo Wiki ya Sheria kwa lengo la kuwajengea uwezo watumiaji wa kufahamu haki na wajibu wao ikiwa ni pamoja na kilitangaza Baraza na kazi zake kwa wadau mbalimbali.



Maafisa wa MORUWASA katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Jumuiya ya Scrappers (vyuma chakavu) walioshiriki kikao kilichoandaliwa na MORUWASA kwa lengo la kuwalimisha madhara yatokanayo na ununuzi wa dira za maji kwa madai ya kuwa ni vyuma chakavu. Picha na Chipegwa Samwel

Wizi wa dira za maji: MORUWASA yaongea na jumuiya ya chuma chakavu

Na Chipegwa Samwel, Morogoro

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imewakutanisha wanachama wa jumuiya ya wafanyabiashara wa vyuma chakavu katika Manispaa ya Morogoro kwa lengo la kuwapa elimu na kuwashamasisha juu ya vita dhidi ya wizi wa dira za maji.

Akifungua kikao hicho kilichopanya kwenye ukumbi wa Kilakala uliopo Jengo la Soko la Chifu Kingalu, Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa MORUWASA Bwana Beno Kiguhe aliwajulisha wana jumuiya ya wafanyabiashara ya vyhuma chakavu wa Manispaa ya Morogoro, Polisi-kata na wadau wengine juu ya kuibuka na kukithiri kwa wizi wa dira na viungio vya mabomba ya maji.

"Kumeibuka wimbi la wizi wa miundombinu ya maji hasa vifaa vya maungio na dira za maji ambapo takwimu zetu zinaonesha kuwa kwa mwezi Januari na Februari 2023 pekee jumla ya dira 80 ziliibwa na hivyo kuisababishia hasara MORUWASA pamoja na watumiaji wa huduma za maji," aliezea ndugu Kiguhe.

Akiongea wakati wa mkutano huo, Msanifu na Mdhifikasi Hujuma wa MORUWASA Bwana Nickson Muta aliezea kuwa miradi ya maji inagharamu fedha nyingi sana na Serikali imekuwa ikijitahidi kuleta maendeleo kwenye sekta hii lakini wizi wa miundombinu umekuwa ukirudisha nyuma juhudhi hizo za Serikali.

Tumebaini kuwa, wezi wa miundombinu ya maji hasa dira ni watoto wadogo, watu wazima na watu wenye uraibu wa madawa ya kulevywa wanaojihusisha na uokotaji wa makopo. Mfano katika maeneo ya Kigulunyembe, muokota makopo mmoja alibainika kuwa na mita kadhaa, tuna "RB" yake na kesi inaendelea na kwamba amekiri mita hizo huziuza maeneo ya Mji Mpya kwa mmoja wa wauza vyuma chakavu," alisema Muta.

Muta alisitisitiza na kuwasihii wanajumuiya hiyo kuwa walinzi wa miundombinu ya maji na kuwasihii wakatae kununua vyuma vinavyotoka kwenye miundombinu ya maji zikiwemo mita.

"Niwaombe sana tusiruhusu kuhujumu au wengine kuhujumu maendeleo ya nchi yetu, bali tuwajibike kutoa taarifa MORUWASA au katika vituo vya Polisi tukiona vitendo vya namna hiyo," alisitisitiza ndugu Muta.

Akiongea wakati wa mkutano huo wakili wa MORUWASA Bi. Tumaini Kimaro aliikumbusha jumuiya hiyo kuwa Sheria namba 5 ya Maji ya mwaka 2019 imenorodhesha makosa, faini pamoja na adhabu zinatokana na hujuma katika huduma ya maji na kuongeza kuwa, adhabu hiyo wakati mwingine huunganishwa na adhabu ambazo zimeainishwa kwenye sheria ya makosa ya jinai pamoja na uhujumu wa uchumi.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo ya maji, kuharibu au kuiba miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira kama vile dira, bomba, viungio, vipuli na mi-

tambo ni makosa na kuwa mtu yeyote akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi laki tano mpaka milioni 50 na kifungo gerezani hadi miaka mitano au vyote viwili kwa pamoja," alisema Wakili Tumaini.

Naye ndugu Hussein Mwembe, mmoja wa wanachama wa jumuiya ya 'Scrappers' aliomba MORUWASA iwave elimu elekezi juu ya vyuma vya MORUWASA ili iwasaide kuvibaini vyuma hivyo.

"Hizi semina ziwe za mara kwa mara, lakini pia MORUWASA mtuelimishe kujua tofauti ya bomba zenu na zile za madukani na mtupe picha ya vyuma elekezi mnavyotumia kama ofisi ili tusinunue vyuma ambavyo vinaibwa kwenu, na wakati mwingine ikiwezekana basi mtumie mabomba ya plastiki na vile vyuma ambavyo hamvitumii mvipige mnada," alisema ndugu Mwembe.

Kwa upande wake mwakilishi wa Jeshi la Polisi, Afande ASP Fadhila Cha-chacha aliwajulisha wadau wa mkutano huo kuwa wameshawakamata jumla ya watuhumiwa 7 na kesi 3 zipo mahakamani tayari na jumla ya mita 3 zimefanikiwa kurudishwa.

"Tunawaomba mjenje tabia ya kutoa ushirikiano na taarifa za uhalifu kwa jeshi la polisi ili ziweze kufanyiwa kazi kwa ucharaka," alisitisitiza ASP Chacha. Nalo Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kupitia ofisi zake za mikoa limefanya uchunguzi mdogo juu ya wizi wa mita kutokana na kuripotiwa na baadhi ya mikoa.

Katika uchunguzi huo, EWURA CCC imebaini kuwa watumiaji wengi wanaabiwa mita na wanalipishwa gharama za kurejeshewa mita hizo ambazo hutofautiana kwa kila Mamlaka ya maji. Kupitia uchunguzi huo baraza lina lengo la kuishauri EWURA namna nzuri ya kudhibiti suala hili kupitia sheria na kanuni zilizopo, kuziboresha na au kuongeza zingine.

Hizi ndizo hatua mchakato mabadiliko bei za maji

Na Geofrey Sokesia, Singida

Katika kutekeleza majukumu yake ofisi ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoa wa Singida imekuwa ikitembelea makundi mbalimbali ya wananchi na kuwapatia elimu juu ya haki na wajibu wao kama watumiaji wa huduma za nishati na maji.

Kupitia majukwaa hayo ya utoaji elimu, EWURA CCC imekuwa ikipokea na kuyafanya kazi maswali na kero mbalimbali zinazohusu huduma za nishati na maji. Miongoni mwa kero au maswali ambayo yamekuwa yakiulizwa mara kwa mara ni pamoja na wananchi kulalamikia bei kubwa za maji. Hata hivyo, pamoja na kulalamikia bei kubwa za maji watu wengi wamekuwa wakiuliza swali la kutaka kujua namna mchakato wa upangaji wa bei za maji unavyofanyika.

Bwana Ibrahim Imbele ni mkaizi wa mtaa wa Kimpungua Manispaa ya Singida, ambaye ni moja ya watumiaji wa huduma ya maji na pia ni miongoni mwa wananchi waliohudhuria programu mojawapo ya uelimishaji juu ya huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibit wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Ndugu Imbele aliuliza swali aktaka kujua utaratibu mzima unaotumika wakati mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zinapotaka kubadili bei za maji.

Makala hii inalenga kutoa elimu juu ya hatua zinazofuatwa na kuzingatiwa katika mchakato mzima wa upangaji na mabadiliko ya bei za maji.

Kwa mujibu wa chapisho la EWURA la tarehe 21.05.2021 linaeleza kuwa upangaji wa bei za maji za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira hufanywa na EWURA kwa kuzingatia Sheria ya EWURA (Cap 414) na Sheria ya Maji namba 5 ya mwaka 2019.

“

EWURA hupitia hatua kuu nne wakati wa kufanya mchakato wa maombi ya mabadiliko ya bei yanayowasilishwa kwake na mamlaka za maji. Hatua hizi zipo ili kuhakikisha kuwa bei zinazopitishwa ni halali, za kweli, zinazokubalika, zinajali makundi yenye kipato cha chini na zitawezesha mamlaka ya maji husika kutoa huduma endelevu

Aidha, kwa kuzingatia Sheria hizo, zipo kanuni za kupanga bei [The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Water Tariff Application and Rate Setting) Rules, 2020] ambazo zinaainisha utaratibu wa marekebisho ya bei.

EWURA hupitia hatua kuu nne wakati wa kufanya mchakato wa maombi ya mabadiliko ya bei yanayowasilishwa kwake na mamlaka za maji. Hatua hizi zipo ili kuhakikisha kuwa bei zinazopitishwa na EWURA ni halali, za kweli, zinazokubalika, zinajali makundi yenye kipato cha chini na zitawezesha mamlaka ya maji husika kutoa huduma endelevu. Hatua hizo ni pamoja na:-

1. Kupokea Maombi

Maombi ya kubadilisha bei za maji huwasilishwa EWURA na mamlaka husika ya maji baada ya

 **MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SHINYANGA**
HAKIKI MFUMO WAKO WA MAJI 



KAMA UNAHISI BILI YAKO YA MAJI NI KUBWA KULIKO UNAVYOTUMIA. FUATA NJIA RAHISI ZIFUATAZO KUJUA CHANZO.

- 1** Funga koki zote za maji
- 2** Angalia mita yako kama bado inazunguka
- 3** Subiri kwa muda wa nusu saa na angalia tena kama mita inazunguka

MATOKEO
Ikiwa mita itaonekana ikizunguka basi ni ishara kuwa kuna mivujo midogo midogo kwenye maungio ya mabomba ya maji.

Facebook: Shuwasa Shinyanga | Instagram: shuwasa_on_insta | Twitter: shinyanga_uwasa

“

Maamuzi ya maombi ya bei mpya hutangazwa kupitia Agizo la EWURA (Tariff Order) kwenye Gazeti la Serikali na katika magazeti ya kawaida. Katika Agizo hilo, EWURA huainisha bayana misingi na hoja zilizozingatiwa katika kufikia maamuzi yake na masharti ambayo mamlaka ya maji husika itatakiwa kuyatekeleza.

kuchambuliwa kwa kina. Maombi hayo huwasilishwa baada ya kupitiwa na kuidhinishwa na Bodi ya Mamlaka husika ya maji. Kwa mujibu wa Sheria ya Maji ya Mwaka 2019, wajumbe wa bodi wa mamlaka za maji ni wawakilishi wa makundi mbalimbali ya wananchi wa eneo husika ambaao ni pamoja na mwakilishi wa madiwani, mku-rugenzi wa mji, mwakilishi watumiaji wakubwa wa maji, mwakilishi wa wanawake na mwakilishi wa watumiaji wadogo wa maji ambao huridhia na hatimaye kuwasilishwa EWURA

Pamoja na mambo mengine, maombi ya mabadiliko ya bei yanayowasilishwa EWURA yanapaswa kuainisha bei zinazopendekezwa, sababu na msingi wa kuomba mabadiliko ya bei na manufaa ambayo wateja na mtoa huduma watahayata kutokana na mabadiliko haya.

2. Kufanya Taftishi

Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414, mara baada ya kupokea maombi, EWURA huanzisha taftishi (inquiry) ambayo inajumuisha kukusanya maoni ya wadau wa huduma zinazotolewa na mamlaka husika. Taftishi inahusisha kutangaza maombi ya bei kwenye vyombo vya habari (Gazeti la Serikali, tovuti ya EWURA, magazeti yanayofika eneo la huduma na mbao za matangazo katika eneo la huduma) ili kupata maoni ya wateja na wadau wa huduma za maji kuhusu bei zinazopendekezwa.

Maoni kupokelewa kwa maandishi kupitia mkutano wa hadhara

ambao hufanywa na EWURA katika eneo linalohudumiwa na mamlaka husika. Pia katika hatua hii, EWURA hypokea maoni kutoka Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC).

Wakati wa kupata maoni ya wananchi kupitia taftishi, wananchi wengi wamekuwa na mawazo kuwa hicho ni kikao cha maamuzi cha kuamua kama bei ipite au isipite. EWURA imekuwa mara kwa mara, wakati wa taftishi ikitoa ufanuzi kuwa, EWURA inachotaka ni sababu za kukataa au kukubali kupandisha bei na nini kifanyike ili kuboresha huduma na siyo kutoa maamuzi katika mkutano wa kukusanya maoni.

Aidha, maamuzi juu ya bei iliyooombwa hufanywa na Bodi ya EWURA kwa kuzingatia sababu za mamlaka husika kuomba kubadilisha bei ya huduma zake, maoni ya wadau na wateja wa mamlaka ya maji husika, na maoni na ushauri wa mabaraza ya ushauri (EWURA CCC na EWURA GCC).

3. Kufanya Tathmini ya Mapendekezo ya Bei

EWURA huidhinisha bei za maji kulingana na gharama za kutoa huduma kwa mamlaka ya maji husika. Gharama hizi huwa ni pamoja na gharama za kila siku za uendeshaji na matengenezo kama vile gharama za uzalishaji wa maji, usafirishaji, usambazaji, watumishi na utawala. Gharama kwa ajili ya kubadili miundombinu iliyochakaa, kuisha muda wake au kuongeza miundombinu kwa ajili ya wateja wa-

pya hutegemea fedha inayotengwa ya uchakavu (depreciation). Gharama zote hizo lazima ziwe zimeainishwa na kuchambuliwa kwa kina katika mpango wa kibiashara (Business Plan) wa mamlaka ya maji kwa kipindi cha miaka mitatu inayoombewa bei mpya.

Jukumu la EWURA ni kupitia gharama na kuona kama zina uhalali na uhalsizia kwa kulinganisha na gharama za kipindi cha nyuma za mamlaka husika pamoja na mhesabu ya fedha yaliyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Gharama hizo hugawanywa kwa wateja wote kulingana na matumizi yao ya maji na ndipo bei za maji kwa kila daraaja la mteja hupatikana.

Aidha, EWURA huzingatia kulinda maslahi ya wateja, huduma kwa wasio na uwezo pamoja na uendelevu wa huduma husika. Vilevile, tathmini ya mapendekezo ya bei huzingatia mlinganisho wa gharama za uendeshaji za mamlaka nyingine za maji hapa nchini zinazotoa huduma ya majisafi na majitaka katika mazingira yanayofanana. Pamoja na maoni ya wateja na wadau kuzingatiwa katika kufikia uamuzi wa bei inayostahili, maoni yao huzingatiwa katika kupitisha bei na pia hutumika kuainisha masharti ambayo mamlaka ya maji itapaswa kuyatekeleza sambamba na bei zitakazoidhinishwa.

4. Uamuzi wa bei

Maamuzi ya maombi ya bei mpya hutangazwa kupitia Agizo la EWURA (Tariff Order) kwenye Gazeti la Serikali na katika magazeti ya kawaida. Katika Agizo hilo, EWURA huainisha bayana misingi na hoja zilizozingatiwa katika kufikia maamuzi yake na masharti ambayo mamlaka ya maji husika itatakiwa kuyatekeleza.

Aidha, Agizo hilo huweka bayana tarehe ambayo bei zilizoidhinishwa zitaanza kutumika na kukoma. Kwa mujibu wa Sheria ya EWURA, mtu yejote ambaye hakuridhika na uamuzi wa EWURA anayo haki ya kukata rufaa kwenye Baraza la Ushindani wa Haki katika Biashara yaani 'Fair Competition Tribunal'.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Upanga wakipatiwa elimu kuhusu Huduma za Nishati na Maji wakati wa programu ya uelimishaji iliyofanywa na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Ilala. Picha na Mpigapicha Wetu

Kamati yaomba ushirikiano kwa Wakuu wa shule

Na Catherine Charles, Dar es salaam

Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkao wa Ilala jijini Dar es salaam ndugu Amiri Nongani amewaomba walimu wakuu wa shule za msingi na Sekondari katika Manispaa ya Ilala kutoa ushirikiano kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) ili kutimiza azma yake ya kutoa elimu inayohusu huduma hizo kwa wanafunzi wa shule zao.

Akizungumza wakati wa programu ya uelimishaji iliyofanywa na Kamati hiyo hivi karibuni katika Shule ya Msingi Upanga, ndugu Nongani alisema kuwa, mara kadhaa wamekuwa wakikosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya walimu wakuu katika suala zima la kupata nafasi za kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Nongani alisema kuwaelimisha wanafunzi kuhusu matumizi bora ya huduma za nishati na maji ni kugenyeza mabalozi kwani wakipata elimu hiyo wataisambaza kwa familia zao, ndugu, jamaa na marafiki na hivyo kusaidia Watanzania wengi kuwa na matumizi endelevu ya huduma za nishati na maji.

"Tukiwapatia elimu hawa wanafunzi naamini wataipeleka elimu hii kwa wazazi na hata kwa majirani zao. Wanafunzi ni rahisi kuishi-ka elimu hii kwani bado hawajawa na majukumu mengi tofauti na sisi watu wazima," alisema Nongani.

Alieenza kuwa wanafunzi pia ni sehemu ya watumiaji wa huduma za nishati na maji katika ngazi ya familia, hivyo wakipatiwa elimu na wakaelewa, watakuwa ni sehemu ya kuendeleza elimu ya matumizi sahihi na endelevu ya huduma.

Alisema watoto mara nyingi wamekuwa wakitumia vibaya huduma za umeme na maji kwa kuwa hawajui ni kwa namna gani wazazi wao wanatumia fedha nyingi kugharlamia huduma hizo, hivyo kwa kuwapatia elimu wanafunzi inaweza kusaidia kupunguza matumizi ya umeme na maji yasiyo na tija majumbani na hata mashuleneni.

Aliwaomba walimu wakuu hao kutoa ushirikiano kwa Baraza pale linapoomba nafasi ya kutoa elimu kwa wanafunzi katika shule zao.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake Jumanne Abdallah alilishukuru Baraza kwa kufika shulenii kwao na kuwaelimisha kuhusu mambo mbalimbali kama vile haki na wajibu wa mtumiaji, vidokezo


muhimu nya matumizi ya huduma za nishati na maji na kueleza kuwa, elimu hiyo imekuwa na manufaa makubwa kwao na kwamba kupitia elimu hiyo watu wengi watanufaika.

"Tunashukuru kufika shulenii kwetu na tunashukuru pia kwa elimu na vipeperushi mlivyotupatia. Tunawaahidi kwenda kuwaelimisha wazazi wetu kuhusu haya tulijoifunza leo, na pia tutawapa hivi vipeperushi mlivyotupatia kwa ajili ya kuvisoma," alisema ndugu Jumanne.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Upanga Bi. Aziza Mbura alilishukuru Baraza kwa kufika shulenii kwake na kuwaelimisha wanafunzi pamoja na walimu wa shule yake kuhudu namna sahihi ya kutumia huduma za nishati na maji.

Aidha aliyahakikishia wajumbe wa Kamati kuwa shule yake itakuwa tayari muda wowote ule pale Kamati hiyo itakapohitaji tena nafasi ya kutoa elimu kwa wanafunzi na walimu.

"Tutawapeka muda na wakati wowote ule mtakapohitaji kuja kutupatia elimu. Mwaka ujao tutapokea darasa la kwanza na darasa la saba waliopo watakuwa wamemaliza shule, hivyo tutawaomba tena mje muwape elimu wanafunzi wetu wapya," alisisitiza Mwalimu Mkuu huyo.



Dira ya maji ikionesha namna ya kusoma mita hizo.

Walia na wasoma mita za maji

Na Josephine Ntaumenya, Mwanza

Baadhi ya wateja wa Mamla-ka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA), wamelala-mikia kitendo cha kutopata ushiriki-anu kutoka kwa wasoma mita za maji na kuomba kuwepo kwa usomaji shirikishi ili kuondoa malalamiko ya ankara za maji.

Wateja hao walitoa malalamiko hayo kwa nyakati tofauti jijini Mwanza, wakati wa utoaji wa elimu kwa watumiaji uliofanywa na Baraza la Usahauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoa wa Mwanza.

Akionesha uwepo wa hali hiyo, mmoja wa watumiaji wa huduma ya maji jijini Mwanza ndugu Elikana Mabula alieleza kuwa, jambo hilo lime-kuwa kero kwani hawajui namna mita hizo zinavyosomwa na kwa wakati gani, lakini hata wanapoonekana wasomaji hao huwa hawatoi maelezo yoyote.

"Ni kero sana kwa kuwa hatujui wanasoma mita saa ngapi, na hata iki-tokea wakafika hawasomi chochote zaidi ya kuangalia tu mita na kuondo-

“

Nyumbani kwangu
wanakuja kusoma
kila mwezi, ila
wakishamaliza
kusoma wanaondoka.
Hakuna elimu yoyote
tunayopewa...

ka, tunabaki hatujui kinachoendelea," alieleza Mabula.

Naye Bi Yunisi Peter mkazi wa Igoma jijini Mwanza, alipouliwa na mwandishi wa habari hii iwapo wasoma mita hao huwa wanafika kusoma mita ya maji na iwapo huwa anape-wa elimu juu ya usomaji mita za maji, alikiri kuwa wasomaji hufika ila hakuna elimu wanayotoa.

"Nyumbani kwangu wanakuja kusoma kila mwezi, ila wakishamaliza kusoma wanaondoka. Hakuna elimu yoyote tunayopewa, na hata hiyo mita mimi sjui kuisoma," alieleza Bi Peter.

Akieleza kuhusu usomaji wa mita

za maji unaofanywa na MWAUWASA, Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja ndugu Meck Manyama, alisema kuwa, kiutaratibu wasoma mita wanatakiwa kutoa elimu kwa wateja.

"Changamoto inayojitokeza ni kuwa mara nyingi wakati wa zoezi la usomaji mita linapofanyika wana-okuwepo nyumbani huwa ni watoto wadogo, wasichana wa kazi za majumbani au wazee sana, ambao hawana uwezo wa kuipokea na kuelewa elimu ya usomaji wa mita," alieleza ndugu Manyama.

Alifafanua kuwa ili kutatta kero hiyo, MWAUWASA imejiwekeea utaratibu ambao hata mteja ambaye hashindi nyumbani anaweza kupata taarifa za usomaji wa mita yake iliyofanuliwa vizuri, na anaweza kujiridhisha na kuwasilisha kero yake kama hataridhika kabla bili ya mwezi husika haijatumwa.

"MWAUWASA tuliliona hili na ili kupata ufumbuzi wake tukaleta utaratibu mzuri ambapo kila baada ya usomaji kufanywa, tunawatumia wateja wetu meseji yenye taarifa za usomaji wa mita ambayo ina ufanuzi wa matumizi ya mwezi husika, ikieleza usomaji uliopita na usomaji wa sasa, uniti alizotumia mteja, na namna ya kuwasilisha malalamiko iwapo ha-jaridhika au kuna makosa kwenye usomaji," alifafanua ndugu Manyama na kuongeza kuwa, kuna muda wa wiki moja wa kuwasiliana na MWAUWASA ili kueleweshwa au kufanya marekebisho kwenye kasoro itakayojitokeza. Baadaye, ujumbe wa pili wa bili ya mwezi husika hutumwa kwa mteja ambayo huchukuliwa kuwa ndiyo an-kara kamili ya mwezi huo.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji ya Huduma za Nishati na maji Mkao wa Mwanza (RCC) ndugu Jimmy Luhende alisema kazi ya utoaji elimu kwa watumiaji itaendelea kufanywa na Kamati kwa kushirikiana na watoa huduma ili kuleta utulivu na usawa kati ya watumiaji na watoa huduma.

"Tunashukuru kwa kuwa watoa huduma wako tayari kushirikiana na Kamati katika kutoa elimu nasi tutaendelea kuwafikia watumiaji ili waendelee kufurahia uwepo wa Baraza na huduma kutoka kwa watoa huduma zilizo bora," alimalizia ndugu Luhende.



Wakazi Rombo wapinga ongezeko bei ya maji

Na Zamda Mabada, Kilimanjaro

Wananchi wa wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, wamepinga pendekezo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo (Rombo WSSA) la kutaka kuongeza bei ya maji kwa wastani wa asilimia 83 kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025.

Pingamizi hilo limetolewa wakati wa mkutano wa taftishi ulioitishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) uliofanyika wilayani Rombo Mkuu mwezi Mei, 2023.

Katika mkutano huo wadau wengi walionesha kupinga upandishwaji mkubwa wa bei ya maji kwa watumiaji wa majumbani yaani toka shilingi 800 bei ya sasa hadi 1,362 kwa bei iliyooombwa kwa "uniti" moja na itaendelea kuongezeka kwa kiasi cha shilingi 100 kila mwaka, kwa miaka mitatu mfululizo.

Wakichangia maoni yao wadau wengi waliitaka Rombo WSSA kutafuta vyanzo vingine vya mapato na sio kutegemea kumuongezea gharama mtumiaji wa mwisho.

"Hili ongezeko la bei ni kubwa sana, sijui wametumia vigezo gani kufikia hapo. Nawashauri wabuni vyanzo vingine vya mapato na sio kutaka kutuumiza sisi watumiaji wadogo," alisema ndugu Onesmo Boyongo mkazi wa Mengwe wilayani Rombo.

Akichangia kwenye mjadala huo Ndugu Epimack Massawe mkazi wa

Mashati alisema kuwa kama Mamlaka inapata ruzuku ya Serikali haina sababu ya kupandisha bei kwa watumiaji.

"Kama Mamlaka inapokea ruzuku kwa nini ipandishe bei wakati hata gharama za kujientesha ni ndogo pamoja na idadi ndogo ya watumishi. Waboreshe kwanza huduma ya upatikanaji maji ndio waje na wazo la kupandisha bei na isiwe kwa kiwango walichoomba," alieleza Ndugu Massawe.

Akitoa maoni ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), Mwenyekiti wa Baraza hilo Mhandisi David Ngula, alisema kuwa, Rombo WSSA inategemea kupata ruzuku ya Serikali inayofikia kiasi cha TZS 16,063,361,875.00 kwa kipindi cha miaka ya 2022/23, 2023/24 na 2024/25, lakini haijajumuisha kiwango hiki cha ruzuku katika ukokotoaji wa makadirio ya bei inayopendekezwa katika miaka husika.

"Ikiwa Serikali inachangia kiasi kikubwa hivi kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa maji Rombo, wananchi wa Rombo wangetegemea kupata unafuu kwenye bei ya maji na si vinginevyo. Tunashauri EWURA kujumuisha viwango hivi vya ruzuku kwenye ukadiriaji wa bei mpya zilizombwa," alisema Mhadisi Ngula.

Alisema kuwa, badala ya Mamlaka kujimbilia kuongeza bei ya huduma, basi itafute njia mbadala za kujiongezea mapato ikiwemo kwa kufanya kazi kwa ufani zaidi kwa kutumia uwezo wa ndani wa Mamlaka ili kuongeza mapato.

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma Nishati na Maji (EWURA CCC) Mhandisi David Ngula, akisoma maoni ya Baraza wakati wa Kikao cha Taftishi kuhusu ombi la kurekebisha bei za maji za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Rombo (Rombo WSSA). Picha na Zamda Mabada

Mhandisi Ngula pia alishauri kuwa "Mamlaka itafute misaada zaidi kutoka Serikalini na kwa wahisani mbalimbali, iimarishe usimamizi na ukusanyaji mapato kutoka asilimia 88 hadi 97 inayokubalika ikiwa ni pamoja na kubana matumizi ya taasisi na kuongeza pamoja na kuendeleza vyanzo vypya vya maji mserereko (gravity) ili kuachana na matumizi ya visima (boreholes). Hii itapelekea kumpunguza gharama kubwa inazotumia kulinipa nishati ya umeme."

Akijibu baadhi ya hoja zilizoibulisha na wadau wakati wa mkutano wa taftishi Kaimu Mkurugenzi wa Rombo WSSA Mhandisi Martin Kinabo alisema kuwa Mamlaka itaendelea kuboresha huduma za upatikanaji wa maji pamoja na ubora wa maji hayo.

"Kwa sasa Mamlaka imeanza kwa kuboresha miundombinu ya maji kama mabomba pamoja na kujenga matenki kwa ajili ya kuhifadhi na kusambaza maji kwa wateja. Tunatarajia pia kuongeza muda wa kutoa huduma kutoka masaa 8 hadi 16 kwa siku," alisema Mhandisi Kinabo.

Akifunga mkutano huo mwakilishi wa Mkurugenzi wa EWURA Mhandisi Lorivii Long'ido aliishukuru hadhara ya mkutano huo kwa kushiriki na kutoa maoni yao na kuwahakikisha kuwa maoni yao yatazingatiwa na yatasaidia katika kufikia muafaka wa bei zilizombwa. Mhandisi Long'ido aliwataka wadau hao kuendelea kutoa maoni yao kwa njia ya maandishi kabla ya tarehe 25/5/2023.

TANESCO yaipa heko EWURA CCC

Na Ramadhan Kakende, Sumbawanga

Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) mkoa wa Rukwa limetoa pongezi na shukrani kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mkoa wa Rukwa kwa kuchangia utekelezaji wa shughuli na malengo ya Shirika hilo mkoani Rukwa.

Shukrani hizo za pongezi zime-tolewa hivi karibuni wakati wa kikao cha majadiliano kati ya TANESCO Rukwa na wateja wakubwa na wa kati wa huduma za umeme katika kikao kilichoandaliwa na TANESCO na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali ikiwemo EWURA CCC na kufanyika mjini Sumbawanga.

Katika kikao hicho, ofisi ya TANESCO ilitoa shukrani kwa wadau wake waliofanikisha utekelezaji wa shuguli zake ikiwemo EWURA CCC, ambayo ilipewa cheti cha uthamini (Certificate of Appreciation) kutoka Shirika hilo la Umeme ikiwa ni utambuzi na kuthamini kazi zinazofanywa na Baraza mkoani Rukwa.

Akizungumza wakati wa utoaji wa cheti hicho, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Rukwa Mhandisi Fedrick

Njavike aliiifu EWURA CCC hasa katika kipengele cha utoaji elimu kuitia semina zake na katika kutafuta suluhisho kwenye malalamiko ya wateja.

"EWURA CCC ni mdau mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa kuwa ni taasisi iliyio karibu na watumiaji na hivyo ni msaada katika kuwafikia wateja wetu. Katika kuwasiliana na wadau wetu, EWURA CCC imekuwa ni kiungo kikubwa na muhimu hivyo pookeni pongezi zetu," alisema Mha Njavike.

Alisema, kuna nyakati ambazo TANESCO na EWURA CCC hupeana changamoto katika utoaji wa elimu zinazohusu huduma ya umeme am-bapo daima EWURA CCC imekuwa msaada mkubwa katika kushiriki kuleta mawazo chanya.

"EWURA CCC pamoja na uelimishaji inaoufanya, imekuwa msaada katika utatuzi wa malalamiko ya wateja wetu, kwa hiyo nawapongeza na naomba tuendelee kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yetu," alimaliza Mhandisi Njavike.

Akipokea cheti hicho cha uthamini, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Rukwa (RCC) Bi. Faustina Vallery ali-shukuru TANESCO kwa kuthamini

mchango wa EWURA CCC na kuahidi kuwa, utambuzi ni chachu ya kuongenza ushirikiano baina ya EWURA CCC na TANESCO ili kuchagiza uboreshwaji zaidi wa huduma za umeme mkoani Rukwa.

"Tunashukuru sana TANESCO kwa pongezi na zawadi hii kwani ni mara chache sana taasisi kuithamini taasisi nyingine hasa kama bidhaa au huduma mnayohusika nayo ni moja. Tunawaahidi kuongenza ufanisi na ushirikiano kati yetu na ninyi katika kuhakikisha watumiaji wanapata huduma bora ya umeme," alisema Bi Vallery.

Aliwasisitiza watumiaji waliohuduria kikao hicho kuhakikisha wanaitumia EWURA CCC kama chombo chao kwa lengo la kutoa maoni, ushauri na malalamiko yao juu ya huduma wanazozitumia hususan zile zinazodhibitiwa na EWURA ambazo ni nishati na maji.

"Niwaombe pia watumiaji mlifika leo muitumie ofisi ya EWURA CCC kwani ipo mahsus kwa ajili yenu katika kutoa maoni, ushauri na malalamiko juu ya huduma za nishati na maji. EWURA CCC inashirikiana kwa ukaribu na watoa huduma kama TANESCO ili kuhakikisha ninyi watumiaji mnapata huduma bora," alimaliza Bi Vallery.

Naye mshiriki wa kikao hicho toka Wilaya ya Kalambo Bwana Lucas Lufite, alisema alikuwa haijui EWURA CCC kama ndio mtetezi wake lakini baada ya pongezi hizo amekitambua chombo hiki na kuahidi kukitumia atakapopata changamoto yoyote inayohusu huduma za umeme.

"Nilikuwa sijui kama EWURA CCC ndio mtetezi wetu sisi watumiaji wa umeme. Leo nimejua kuwa Serikali inatupenda na kututengenezea chombo chetu kiweze kututetea. Nimem-sikia vizuri Bi Vallery akisema kuhusu kazi za EWURA CCC, niwaahidi kuwa kuanzia sasa sitasita kuleta malalamiko yangu na wenzangu tutakopata changamoto ya huduma," alisema Lufite.

EWURA CCC imekuwa ni chombo kinachowaleta pamoja watumiaji na watoa huduma hasa kwa kuitia semina za uelimishaji inazoianda, lakini pia katika kusimamia na kuhakikisha haki na wajibu wa watoa huduma na watumiaji vinazingatiwa ili kudumisha ubora wa huduma za nishati na maji.

Pongezi



Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga Mjini Mheshimiwa Sixtus Mapunda (Kushoto) akimkabidhi cheti cha uthamini Bi Faustina Vallery (Kulia) Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Rukwa kwa niaba ya EWURA CCC, kilichotolewa na ofisi ya TANESCO mkoani wa Rukwa kwa lengo la kutambua mchango wa Baraza katika kuwaelimisha watumiaji wa huduma ya umeme mkoani Rukwa. **Picha na Ramadhani Kakende**

Waaswa kulalamikia huduma mbovu

Na Geofrey Sokesia, Singida

Wito umetolewa kwa wakazi wa Mtaa wa Unyakahe Manispaa ya Singida kutokukaa kimya na badala yake kupaza sauti kwa kulalamikia huduma mbovu zinazotolewa na watoa huduma wa maji na nishati katika Manispaa hiyo.

Wito huo umetolewa hivi kari-buni na Mwenyekiti wa Mtaa wa Unyakahe Manispaa ya Singida ndugu Abubakari Athuman wakati wa mukutano na wananchi wa mtaa huo amba Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) lilishiriki kwa lengo la kutoa elimu.

Akizungumza wakati wa kia-kao hicho, bwana Athuman alise-ma kuwa, wakazi wa mtaa wake wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali zinazohusu huduma za nishati na maji lakini wameku-wa wakikaa kimya pasipo kupe-leka malalamika yao mahali popote pale.

"Wananchi wa mtaa wangu wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali zinazohusu huduma za maji na nishati lakini wengi wao wamekuwa wanakaa kimya na kuendelea kuvumilia kutokana na utamaduni wa kushindwa kupeleka malalamiko kwenye mamlaka husi-

ka," alisema Athuman.

Alitaja moja ya sababu ya kuto-kulalamikia huduma mbovu kuwa ni pamoja na kukosa uelewa wa haki na wajibu wao na hivyo kubaki bila msaada wala utatuvi wa changamoto zitokanazo na huduma dunii.

"Kuna watu wengi wameathirika na utamaduni wa kuogopa kuishitaki taasisi ya Serikali wakiamini kuwa labda wanawenza wakasitishiwa huduma au wao kushitakiwa mahakamani," alisema ndugu Athuman na kuongeza kuwa, wananchi wengi huungiwa na woga kufikisha malalamiko kwenye vyombo vya haki kwa imani kuwa, kufanya hivyo kunaweza kuwasababishia matatizo."

Akitoa ushuhuda wake, ndugu Mikidadi Shabani mkazi wa mtaa wa Unyakahe aliwaasa wananchi wen-zake wa mtaa huo kuondoa dhana ya woga wa kulalamikia huduma mbovu zinazotolea na watoa huduma za nishati na maji na kuwashauri panapokuwa na uhitaji wa shirikishe ofisi ya EWURA CCC, kwa kuwa Baraza hilo kuitia ofisi yake ya Singida liliwahi pamoja na maeneo mengine kusaidia katika utatuvi wa changamoto ya kucheleweshwa kuunganishiwa huduma ya maji.

"Mimi niliomba kuunganishiwa huduma ya maji lakini sikupata huduma hiyo kwa wakati hivyo niliamua bila woga wowote kufikisha

alamiko langu ofisi ya EWURA CCC Singida na ndipo walinisaidia kwa kujaza fomu ya malamiko ya EWURA na hatimaye lalamiko langu lili-patiwa ufumbuzi nami nikapata huduma ya maji haraka," alifafanua ndugu Shabani.

Kwa upande wake Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Singida Bi. Evarista Lucas alishaombwa wananchi wa mtaa wa Unyakahe kujenga tabia ya kulalamikia huduma mbovu, huku akiwasitisitiza kwa kuwaeleza kuwa, EWURA CCC ni taasisi ya Serikali na ipo kisheria kuwatumikia wananchi kwa kuwatetea pale haki zao zinapokiukwa.

"Msigope kuitumia EWURA CCC Singida na pia msigope ku-lalamikia huduma mbovu. Mkikaa kimya watoa huduma wataendelea kutoa huduma chini ya viwango na hivyo mtakaoumia ni nyie wananchi," Alisisitiza Bi Lucas.

EWURA CCC kuitia ofisi yake mkoani Singida itaendelea na programu yake ya uelimishaji kwenye mitaa na kata mbalimbali ndani ya Manispaa ya Singida kwa lengo la kuwajengea uwezo watumiaji wa huduma za nishati na maji ili wazitambue haki zao na kuzidai pale wanapoona zimeminywa ili kuwa na mchango katika kuboresha huduma za nishati na maji mkoani humo.



Bi Everista Lucas (wa kwanza kushoto), Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Singida akisikiliza kwa makini swali kutoka kwa mmoja wa washiriki wa mukutano wa wananchi wa mtaa wa Unyakahe Manispaa ya Singida. Picha na Mpigapicha Wetu

Wizi wa dira/mita za maji wakithiri

Na Zamda Mabada, Kilimanjaro

Kwa miezi ya hivi karibuni kumekuwepo taarifa za wananchi wa Manispaa ya Moshi kuibwa mita za maji majumbani mwao. Taarifa hizi zimekuwa zikitolewa na wateja waliopo maeneo mbalimbali katika manispaa ya Moshi ambao wana-hudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Moshi (MUWSA).

Dira/mita ya maji ni kifaa kinachotumika na mamlaka za maji nchini kupima kiasi cha maji amba-cho mteja ametumia. Mamlaka za maji huzifunga mita hizi kwa wate-ja wake wa makundi yote, na mara nydingi hufungwa nje ya nyumba za wateja mahali ambapo itakuwa rahi-si kwa wafanyakazi wa mamlaka kuziona na kuzisoma. Wakala wa Vipimo (WMA) anawajibika katika kuhakikisha usahihi wa mita hizi zinazotumiwa na mamlaka za maji.

Ni muhimu mteja kufungiwa mita ya maji ili kupata usahihi wa matumizi yake kwa muda wa mwezi badala ya kupata ankara za makadi-rio.

Kwa mujibu wa takwimu za MUWSA kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Mei 2023 jumla ya dira arobaini na mbili (42) ziliwbwa.

Wizi wa mita za maji unaofanya-wa na watu wasio waaminifu ume-kithiri na kusababisha usumbufo kwa wateja pamoja na kuleta hasara kwa MUWSA na Serikali kwa ujum-la.

Serikali inatumia fedha nyingi kuhakikisha huduma ya maji inapati-kan kwa wananchi na hivyo kwa mujibu wa Sheria ya huduma ya maji na usafi wa mazingira Na. 5 ya mwa-ka 2019 inaweka marufuku mtu yoyote kuhujumu miundombinu ya maji.

Uchunguzi mdogo uliofanywa na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya Mkoa wa Kiliman-jaro (RCC) umegundua kuwa kuna sababu 2 zinazochochea wizi wa mita za maji ambazo ni pamoja na:-

- Uuzaji wa vyuma chakavu ili kujipatia kipato; na

- Udanganyifu wa mteja mwenye deni kubwa kwenye dira yake an-yeamua kulipoteza deni hilo ili kusi-wepo na ushahidi wa "uniti" zilizotu-mika kwenye dira yake.

Madhara yanayoweza kusaba-bishwa na wizi wa dira

- Ukosefu wa huduma ya maji kwa mteja ambaye mita yake imeib-wa kutokana na kusitishiwa huduma hadi dira mpya itakapoletwa.

- Ukwamishaji wa shughuli za ki-maendeleo kwani mamlaka ya maji hujikuta ikinunua mita mara kwa mara badala ya kuendelea kujenga miundombinu mipy kwa ajili ya wateja wapya wa maji; na

- Kuongeza gharama za kununua dira mpya ili kurudishia zile zilizopo-tea badala ya kushughulika na hudu-ma zingine kama vile maunganisho mapya na kubadilisha zilizo chakavu na si zilizoibwa.

Nini kifanyike?

- i. Mamlaka zijenge na kuboresha chemba za kuhifadhi mita ambapo zitafungwa na kuzifungia kwa kufu-li au komeo ili kuzuia wizi usijirudie tena;

- ii. Mamlaka ya maji Moshi kwa kushirikiana na watendaji wa kata na mitaa ihakikishe inawaelimisha wateja wake kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya maji ili kuepuka hasara kwa Mamlaka na madhara kwa watumiaji wa maji;

- iii. Mamlaka iboreshe mahusiano kati yake na wateja ili kupata taari-fa za uhujumu wa miundombinu ya maji; na

- iv. Mamlaka itoe motisha kwa watoa taarifa juu ya wahujumu wa miundombinu ya maji.

- v. Watumiaji wawe wazalendo kwa kulipa bili zao kwa wakati ili kuepuka malimbikizo yanayozaa deni kubwa na hatimaye kuweza kuleta ushawishi wa kuharibu/kuiba dira kwa lengo la kupoteza ushaidi wa uniti zilizotumika.

Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 kifungu cha 61 kinabainisha "kosa la kuharibu miundombinu ya maji adhabu yake ni faini ya milioni tano (Tsh. 5,000,000) na isiyozidi milioni hamsini (Tsh. Milioni 50) au kifungo cha kati ya miaka miwili hadi mitano jela au vyote kwa pamoja.

Watumiaji wa maji wanataki-wa kutambua kuwa maji ni uhai na uhai unategemea maji, hivyo basi ni vyema wakaitunza miundombinu ya maji hasa dira ili kuepusha ukosefu wa huduma hii muhimu kwa binada-mu na viumbe hai wengine.



Changamoto



Watumiaji na wadau mbalimbali wa huduma ya maji mkoani Rukwa wakiwa katika kikao cha Taftishi kilichoitishwa na EWURA hivi karibuni kwa lengo la kujadili maombi ya SUWASA ya kutaka kurekebisha bei ya maji Picha na Mpigapicha Wetu

Waomba mradi wa maji toka ziwa Tanganyika

Na Mwandishi wetu, Sumbawanga

Wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga wameombia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga (SUWASA) kuanzisha mradi wa maji utakaotoa maji Ziwa Tanganyika na kusambaza kwenye makazi ya watu ili kupunguza gharama za maji kwa wananchi pamoja na kuongeza kipato kwa Mamlaka na hivyo kumudu kuijidesha kiuchumi pasipo kutegemea kupandisha bei za maji kwa watumiaji mara kwa mara.

Ombi hilo liliwasilishwa hivi kari-buni wakati wa mkutano wa kutoa maoni (Taftishi) kwa wadau wa maji juu ya maombi ya SUWASA ya kurekebisha bei za maji kwa miaka mitatu mfululizo ulioitishwa na Mamlaka ya Udhibili wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ambao ulifanyika mjini Sumbawanga na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali likiwemo Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji

(EWURA CCC).

Wakitoa maoni yao wadau hao wa huduma za maji baada ya wasilisho la SUWASA, wengi walikataa upandishaji wa bei za maji na badala yake wakaitaka SUWASA kuwa wabunifu kwa kubuni miridi ya maji itakayoongeza kipato kwa Mamlaka pamoja na upatikanaji wa maji ya uhakika kwa watumiaji.

Fred Nkoswe mkazi wa mtaa wa Bomani A' alisema kuwa pamoja na kuwa SUWASA kuomba bei mpya kulingana na gharama za uendeshaji kupanda, inashauriwa Mamlaka hiyo kuwa wabunifu kwa kutoa maji ziwa Tanganyika na kuyasambaza kwenye makazi ya watu, kwa kufanya hivyo kuitapunguza utegemezi wa kipato toka kwa watumiaji kwani ziwani maji ni mengi na hivyo hakutakuwa na uhaba wa maji kwa wakati wote.

Naye Bi Grace Kabelege mkazi wa Kizwite Sumbawanga alisitisiza uwezekano wa kutoa maji Ziwa Tanganyika upo kwa kulinganisha na Mradi wa

Maji wa Ziwa Victoria ambao unapeleka maji mikoa ya Shinyanga na Tabora, hivyo kuiomba SUWASA kufanya tathmini juu ya hilo ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa maji mkoani Rukwa.

"Mimi kwa uelewa wangu naona uwezekano wa kutoa maji Ziwa Tanganyika upo kwani kama imewezeekana kutoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka mikoa ya Shinyanga na Tabora, hapa inashindikanaje?" alihaja Bi Kabelege.

Akijibu hoja hiyo, Mkurugenzi wa SUWASA Mhandisi Gibon Nzowa ali-wataarifu wananchi kuwa, mpango wa kutoa maji Ziwa Tanganyika tayari unafanyiwa tathmini na wataalamu toka Wizara ya Maji, na baada ya tathmini hiyo taarifa ya wataalamu hao itafanyiwa kazi na kutolewa maamuzi na Wizara.

"Naomba niwaambie wadau wetu kuwa mpango wa mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika tayari unafanyiwa kazi na wataalamu toka Wizara ya Maji kwa kufanya tathmini ya kina ya mradi na kuwasilisha majibu yake katika ngazi ya maamuzi," Alieleza Mha. Nzowa.

Alisema miridi kama hiyo ya kutoa maji Ziwa Tanganyika inahitaji tathmini ya kina kabla ya utekelezaji wake kwani ni mikubwa sana katika uendeshaji wake na pia katika kuwashudumia wananchi, na kuwaomba wananchi hao kuwa na subira wakati wa kukamiliisha zoezi hilo la tathmini.

Naye Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala kutoa EWURA CCC Rukwa ndugu Ramadhan Kakende alisisitiza watumiaji kuwa na msukumo mkubwa hasa katika utoaji wa maoni na ushauri juu ya mpango wa mradi huo ili kuzisaidia Mamlaka ikiwemo SUWASA na Wizara ya Maji katika kuharakisha utekelezaji wake.

Aliiomba SUWASA kuongeza nia na jitihada juu ya mpango huo ili kuongeza msukumo kwa Mamlaka husika katika kufanya maamuzi chanya juu ya mradi huo utakaokuwa ni msaada mkubwa kwa wakazi wa Rukwa na mikoa ya jirani.

Mkoa wa Rukwa umezungukwa na vyanzo vingi vya maji japo kiuhalisia vyanzo hivi vimeduwa na mchango mdogo kwa wahitaji wa maji hasa watumiaji wa majumbani, hivyo kama mpango wa mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika utatekelezeka utaenda kuubadilisha mkoa katika suala zima la upatikanaji wa huduma ya maji.

Mambo yanayoweza kuchangia ankara za maji kuwa kubwa

Na Mwasiti Athuman, Mbeya

Kumekuwa na malalamiko mengi toka kwa watumiaji wa huduma ya maji kuhusu ankara za maji kuwa kubwa na hivyo kuleta sintofahamu juu ya jambo hilo ambalo ni kero kubwa kwa watumiaji.

Makala hii inakusudia kuangazia mambo machache muhimu ambayo yanaweza kupelekea ankara za maji kuongezeka, lengo likiwa ni kuongeza uelewa kwa watumiaji wa huduma za maji kubaini chanzo kinachoweza kusbabisha ankara za maji kuwa kubwa na hivyo kuwa kwenye nafasi nzuri ya kue-puka jambo hilo.

1. Mivujo ya maji baada ya mita

Mivujo ya maji baada ya mita huchangia kwa kiasi kikubwa ankara za maji kuwa kubwa na kumuongezea mtumiaji gharama bila kujua. Ifahamike kuwa, kila tone linalopita katika mita huhesabiwa, hivyo maji yote ambayo hupita katika mita huhesabiwa pasipo kujali ni kwa namna gani maji hayo yalitumika. Mivujo hii inawezekana ikapuuzwa kwa kuwa ni midogo, lakini huzalisha lita na lita na hatimaye kukamilisha uniti za maji. Zifuatazo ni aina za mivujo ambayo inaweza tokea kwenye mifumo ya maji majumbani.

a) Mivujo inayoonekana

Mivujo hii ndio ambayo huonekana ikitoa maji kidogo kidogo sana na watumiaji kuipuuza kwa kudhani haiwezi kuleta madhara, lakini mivujo hii isiposhughulikiwa huongezeka siku hadi siku. Mivujo ya aina hii inaweza kuongezeka hususani nyakati za usiku kutookana na msukumo (presha) wa maji kuwa mkubwa zaidi.

b) Mivujo isiyonekana

Mivujo hii hutokeea katika mifumo ya maji baada ya mita hususani katika mabomba yaliyopita chini ya ardhi na kutoonekana kwa urahisi na mtumiaji. Mivujo ya aina hii huendelea kupoteza maji pindi mteja anapotumia maji bila kukoma. Kutookana na ugumu wa maeneo hayo kuonekana kwa macho huendelea kuzalisha matumizi ya maji kwa mteja bila kujua.

Suluhisho

Inashauriwa kuziba mivujo yote inayojitekeza baada ya mita pasipo kujali ukubwa au udogo wake. Mtumiaji anaweza kuwasiliana na fundi bomba ili afanye

ukagazi wa miundombinu ya maji katika jengo husika ili kujiridhisha kuwa hakuna maji yanayopotea. Pia inashauriwa ku-hakikisha unafunga koki za maji za ndani kwa usahihi na ile koki iliyopo nyuma ya mita ili kuzuia upotevu wa maji.

2. Matumizi mabaya/holela ya maji

Matumizi mabaya ama holela ya maji katika makazi hupelekea ankara za maji kuwa juu. Matumizi haya ni kama vile kupiga mswaki, kufua nguo, kuoga, kum-wagilia bustani, kuosha vyombo kwa maji tiririka kutokea katika bomba la maji moja kwa moja n.k. Ijapokuwa matumizi tajwa hapo juu ni ya muhimu, kusipokuwa na uangalifu yanaweza kusbabisha ankara kubwa ikiwa mtumiaji hatakuwa akipima/ratibu kiasi cha maji anachotumia. Mfano, kwa kutumia moja kwa moja maji kutoka kwenye bomba mtu anaweza kujikuta ametumia karibia ndoo nzima ya maji kusu-zazikombe au kupiga mswaki tu.

Suluhisho

Wateja wanashauriwa kuteka maji katika vyombo na kufanya shughuli zao pasipo kutumia maji yanayotirirka moja kwa moja toka katika bomba.

3. Usomaji wa dira za maji usio sahihi

Kulingana na baadhi ya mita kuwa katika maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi au ukosefu wa uadilifu wa baadhi ya wasoma mita, inaweza kutokea dira ya maji imesomwa vibaya au kukadiria-wa matumizi bila msomaji kufika eneo la mita na kusbabisha kuandika uniti ambazo siyo sahihi. Kwa namna hii, ankara ya mteja inaweza kukadiria chini au juu zaidi ya matumizi halisi.

Suluhisho

Inashauriwa kuwa kila mtumiaji ajifunze na aelewe kusoma dira yake ya maji kwa usahihi na namna ankara zinavyo-kokotolewa. Waweza kutembelea ofisi za mamlaka za maji au ofisi za Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ambapo elimu hii hutolewa bure. Pia inashauriwa kwamba, kila upokeapo ujumbe kuwa dira yako ya maji imesomwa, basi nenda kajiridhisho kwenye dira yako kuona kama usomaji huo ni sahihi kabla ankara yako hajaandalawi.

4. Ongezeko la matumizi ya maji katika familia

Inapotokea ongezeko la watumiaji wa

maji katika familia/kaya ndani ya mwezi/miezi husika ankara inaweza kubadilika kwa mteja husika. Ongezeko hilo linawenza kuwa ni pamoa na uwepo wa sherehe, wageni, nyakati za likizo za shule, uzazi n.k. Mambo haya yanaweza kusbabisha ongezeko la matumizi ya maji tofauti na awali na hivyo kuleta mabadiliko ya ankara.

Suluhisho

Kwa uwepo wa watumiaji wengi katika familia, sisitiza uangalifu kwa matumizi ili kujiepusha na ankara kubwa isiyotarajiwa. Hii inahusisha kuwa mwangalifu kwa watoto ambaa baadhi hupenda kufungua maji kwenye bomba na kufurahia yanapotiririka.

5. Ubovu wa dira za maji

Dira za maji ni mashine ambazo hutumika kupima kiasi cha maji yanayotumika kwenda kwa mteja. Hata hivyo, mashine hizi zinaweza kupata hitilafu kama mashine zingine ambapo utendaji wake hupungua au kuharibika na kutoa vipimo visivyo sahihi. Kwa mfano dira hizi zinaweza kusimama na kutokusoma kabisa kiasi chochote cha maji hivyo kupelekea mtoa huduma kupata hasara, au mita hii kuanza kusoma tofauti kiasi cha maji kinachopita au kupima presha/upepo unapopita na kumuongezea mteja gharama ambazo si sahihi.

Suluhisho

Panapokuwa na mashaka juu ya ufanisi wa mita, basi inashauriwa ku-peleka maombi ya kufanyiwa ukagazi wa mita hiyo kwa mamlaka ya maji husika. Ikiwa mita yako itakutwaa ina hitilafu basi mtoa huduma atapaswa kuibadilisha na kurekebisha bili husika. Hata hivyo ikiwa hutardhiswa na majibu ya mtoa huduma kuhusi mita yako, unaweza kuipeleka mita hiyo kwa Wakala wa Vipimo (WMA) kwa uhakiki zaidi.

Ushauri wa jumla

Na vema jamii ikaendelea kujielimisha juu ya changamoto mbalimbali zinazotokana na ankara kubwa za maji na jinsi ya kuzitatu ili huduma hizi ziendelee kuwa endelevu kwa vizazi vijavyo. Watumiaji pia wanashauriwa kulalamika pale wanapokuwa hawaridhishwi na huduma za maji hususani usahihi wa mita zao au bili kubwa ili waweze kulipia huduma kulin-gana na matumizi yao halisi.

Uelimishiha

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Swali: Je, mteja anaweza kurudishiwa uniti zake za umeme endapo mita ya umeme imeungua ikiwa na salio la uniti za umeme?

Ndio. Kwa kuwa ununuzi wa umeme hufanyika kwenye mfumo wa kununua umeme wa TANESCO, taarifa za mteja haziwezi kupotea hata kama mita imeungua. Kwa hiyo ikiwa mita ya mteja imeungua, TANESCO huangalia kwenye mfumo na kujua ni kiasi gani cha uniti zilizokuwepo na atarudishiwa.

Swali: Je, ni wapi mtumiaji anaweza kupata orodha ya mafundi wa umeme wenye leseni ya EWURA kama akitaka kufanya matengenezo au kuangalia mfumo wa waya kwenye nyumba?

Orodha ya mafundi wa umeme wenye leseni ya EWURA unaweza kuiptaki kila ofisi za TANESCO kokote Tanzania bara, au kupertia toyoti ya EWURA (www.ewura.go.tz)

Swali: Je, mteja wa huduma ya maji ana wajibu gani pindi dira ya maji ikiibwa au kupotea?

Dira ikipotea au ikiibiwa mteja anawajibika kufanya yafuatayo:-

- Mosi, mteja anatakiwa atoe taarifa ya wizi au upotetu huo katika kituo cha Polisi na kupatiwa hati maalumu ya kupotelewa kwa mita;
- Pili, mteja anapaswa kutoa taarifa ya wizi wa dira (Loss report) kwa mamlaka husika ya maji inayompatia huduma ili apatiwe dira nyingine.

Swali: Je, nakala ya mkataba wa huduma kwa wateja hutolewa kwa watumiaji wa aina gani?

Nakala ya mkataba wa huduma kwa wateja TANESCO au wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira

hutolewa kwa makundi yote ya watumiaji wa huduma hizo.

Swali: Je, Harufu inayotoka kwenye gesi ya matumizi ya nyumbani inatokana na nini na je haina madhara kwa binadamu?

Gesi ya kupikia majumbani (LPG) huwekewa harufu maalumu ili kumsaidia mtumiaji kujua kama gesi inavuja au inakaribia kuisha. Harufu hiyo haina madhara yoyote kwa binadamu.

Swali: Je, Endapo mita ya maji ya mteja itapimwa na kukutwa ni mbovu mteja ana haki zipi?

Kwa kuwa Kanuni ya 40 ya Kanuni za Kanuni za Ubora wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020 inaelekeza kuwa jukumu la kuhakikisha kuwa mita ni nzima ni la mtoe huduma, hivyo ikiwa mita ya mteja itakuwa ni mbovu basi mteja ana haki ya kubadilishiwa mita hiyo na kufungiwa mita iliyo nzima.

Swali: Je, mtu yeyote anaweza kujaza fomu ya malalamiko ya EWURA?

Fomu ya malalamiko ya EWURA hujazwa na mtu yeyote mwenye malalamiko yoyote yanayohusu huduma za nishati na maji. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni za Utatuza wa Migogoro za Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA) GN no: 428 za mwaka 2020, Kanuni No. 4(1) na (2). Pia Kanuni hizo zinaruhusu EWURA CCC au kikundi cha watu kujaza fomu hiyo.

Swali: TANESCO APP ni nini?

TANESCO APP ni mfumo wa kimawasiliano ambao umetengenezwa na TANESCO ili kurahisisha na kuboresha upokeaji wa taarifa kutoka kwa

Maswali ya ulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

wateja wake. Mteja anaweza kupakua mfumo huu kuitia "Playstore au App-Store" kwa simu janja yake.

Swali: Je ni huduma gani mteja anaweza pata toka kwenye TANESCO APP?

Mteja anaweza kupata huduma zifuatazo akiwa na TANESCO APP ;

- Kutuma maombi ya kuunganishiwa huduma ya umeme
- Kutoa malalamiko
- Kutoa taarifa ya dharura
- Kufanya maulizo kuhusu huduma za umeme

Swali: Je, ni ndani ya muda gani bili ya maji inatakiwa iwe imelipwa?

Kanuni namba 51- (1) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020 inaeleza kuwa mteja wa huduma ya maji anatakiwa awe amelipa bili yake ndani ya siku 30 tangu siku aliyopewa bili. Zaidi ya hapo mtoa huduma anaweza kusitisha huduma ya maji kwa mteja husika.

Swali: Endapo mteja amelipa zaidi ya deni la bili ya maji analodaiwa, Je mteja huyo anaweza kurudishiwa hela yake iliyozidi?

Ndiyo, Kanuni namba 53 - (1) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Mwaka 2020 zinatoa haki kwa mteja aliyelipa zaidi kurudishiwa pesa zake. Aidha, mtoa huduma atapaswa kumlipa pesa taslimu iliyozidi au, kulingana na utashi wa mteja, kumpa uniti za maji mteja huyo kwa thamani ya pesa iliyozidi kuitia namba ya akaunti yake ya maji.

Swali: Je, kuna fidia anayolipwa mteja aliye katiwa maji kimakosa na Mto Huduma?

Ndiyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1) ya Kanuni za Ubora wa Hudu-

ma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2020, Tangazo la Serikali Na. 849 inaeleza "endapo mtoa huduma atamsitishia mteja huduma kimakosa atatakiwa kumlipa fidia. Fidia hii inaweza kuwa ni malipo ya fedha taslim au inaweza kuwekwa kwenye akaunti ya mteja, Kanuni ya 57(2).

Swali: Je ni muda gani TANESCO hutumia kujibu maulizo au malalamiko ya maandishi ya mteja?

- Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO wa mwaka 2006 unaeleza kuwa, maulizo ya maandishi yatajibiwa ndani ya siku 5 za kazi na maulizo yote yatatatuliwa ndani ya wiki moja tangu kupokelewa kwake.

- Malalamiko ya mteja yaliyowasilishwa kwa maandishi yatajibiwa kwa maandishi ndani ya siku 3 za kazi na tatizo litatafutiwa ufumbuzi ndani ya mwezi mmoja

Swali: Je, vituo vya mafuta vinaweza kuza mafuta kwa kiwango chochote cha bei?

Hapana. Vituo vya mafuta huuza mafuta kwa mujibu wa bei kikomo ambazo hutangazwa na EWURA kila Jumatano ya kwanza ya mwezi.

Bei za mafuta hupangwa kwa mujibu wa K kanuni za EWURA za Upangaji wa Bei za Mafuta za mwaka 2022, zikisomwa pamoja na marekebisho ya Kanuni hizo za mwaka 2023 yaani Kanuni za Kurekebisha Bei za Bidhaa za Petroli), marekebishi ya mwaka 2023.

Swali: Je ni muda gani EWURA wanatanga bei mpya za mafuta?

Kwa mujibu wa Kanuni za Upangaji wa Bei za Mafuta za EWURA za Mwaka 2022, Tangazo la Serikali Namba 57 zikisomwa pamoja na marekebishi ya Kanuni hizo za mwaka 2023 yaani

Maswali na Majibu

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Kanuni za Kurekebisha Bei za Bidhaa za Petroli), marekebisco ya mwaka 2023 bei zinapangwa kwa kutumia kikokotoo.

Bei elekezi mpya za mafuta zintangazwa kila Jumatano ya mwanzo wa mwezi katika magazeti yanayowafikia wasomaji wengi nchini, moja likiwa la Kiswahili na moja la Kiingereza. Pia watumiaji wanaweza kupata bei elekezi za mafuta kuitia simu zao kwa kupiga $*152*00*$ au kuitia tovuti ya EWURA ambayo ni www.ewura.go.tz. Nakala ya bei hizo pia zinapatikana kwenye ofisi za EWURA CCC za mikoani na makao makuu.

Swali: Je, ni muda gani natakiwa kulalamika EWURA kama mtoe huduma ameshindwa kuniunganishia huduma kulin-gana na utaratibu uliowekwa?

Lalamiko la namna hii linapaswa kuwasilishwa si zaidi ya miezi kumi na mbili tangu kucheleweshwa huko kutokee. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni za Utatuzi wa Malalamiko za EWURA za mwaka 2020 (EWURA Consumer Complaints Settlement Rules, 2020) Tangazo la Serikali Na.428.

Swali: Je, ni lazima vituo vya mafuta kuwa na mabango ya tahadhali (warning sign)?

Ndiyo. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni za Mafuta za Mwaka 2022 (The Petroleum (wholesale, storage, retail and consumer installation operations) Rules, 2022), Kanuni ya 46(1) ambayo inavitaka vituo vya mafuta kuwa na mabango ya tahadhali ili kuwasaidia wateja na wageni

wanaofika kupata huduma kufahamu nini wanatakiwa na nini hawatakiwi kufanya katika eneo la kituo cha mafuta. Hii inasaidia kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza pasipo kutarajiwa.

Swali: Je, uniti moja ya maji ni sawa na lita ngapi za maji?

Uniti moja ya maji (one cubic meter) ni sawa lita za maji elfu moja, ambazo ni sawa na ndoo 50 za ujazo wa lita ishirini. Hii ni kwa mujibu wa vipimo au mfumo wa "metric."

Swali: Kwa nini mitungi ya gesi huvishwawa wavu?

Kwa mujibu wa Kampuni ya Orxy mitungi ya gesi huvalishwa wavu ili kusaidia kupunguza misuguano kati ya mtungi mmoja hadi mwingine inapokuwa inasafirishwa au inapokuwa mahali pamoja.

Swali: Kwa nini mafuta yatokanayo na Petroli huwa na rangi tofauti tofauti?

Kwa mujibu Titus Kaguo Meneja Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Mafuta huwekwa kemikali maalum kwa jina la "DNA" au vinasaba ili kuttambua mafuta ambayo yanasafrishwa nje ya nchi na ambayo yamelipiwa ushuru kwa ajili ya biashara ndani ya nchi.

Swali: Je, watu binafsi wanaruhusiwa kuomba leseni ya kuzalisha na kusambaza umeme?

Ndiyo. Kanuni za Umeme (Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme) za 2019 Kanuni ya 4 na zikisomwa pamoja na Kanuni ndogo (a), (b),

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

na (c) zinasema mtu yejote anaweza kuomba leseni kutoka EWURA kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza umeme. Hata hivyo, ni lazima awe na barua ya kutambuliwa na usaidizi wa Wizara yenye dhamana na umeme.

Swali: Ni nini tofauti iliyopo kati ya EWURA na RUWASA?

EWURA na RUWASA zinatofautiana kulingana na dhumuni la uwanzishwaji wake. Sheria ya Maji Namba 5 ya 2019 kifungu cha 42(1) kinatambua RUWASA kuwa ni Wakala wa Maji Viji-jini ilhalii Sheria ya Udibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya mwaka 2002 sura ya 414 kifungu cha 4 kinaitambulisha EWURA kuwa ni Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Nishati na Maji.

Swali: Je Mto huduma anaweza akatua lalamiko mara tu lalamiko linapowasilishwa EWURA?

Ndiyo. Mto huduma anaweza kutatua lalamiko mara tu anapopata barua ya EWURA (Samansi) inayomtaka atoe utetezi juu ya lalamiko lililowasilishwa dhidi yake kabla ya kufanyika kwa kikao cha kutafuta muafaka. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, jukumu la kutatua malalamiko ya wateja ni la msingi kwa kila mto huduma, kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma kwa Wateja.

Swali: Ni nani mwenye mamlaka ya kutatua migogoro ya huduma za maji na nishati?

Sheria ya EWURA Sura 414 kifungu cha 29, na 34 pamoja Kanuni

za EWURA za Utatuzi wa Migogoro za mwaka 2020 zinaeleza wafuatao wanaweza kutatua malalamiko ya mtumiaji wa huduma za Nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA:-

- Mto huduma (huduma za Nishati au maji)
- Mdhibiti (EWURA)
- Baraza la ushindani (FCT)

Swali: Kwa njia ipi mteja anaweza kupima mtungi wa gesi kwa kutumia mizani?

Kanuni ya Uuzaji wa Gesi za Kupikia Majumbani GN 222(2013) kifungu no 6, inamtaka muuzaji kuwa na mzani wa kupimia gesi na mzani uwe umehakikisha.

Mtungi kwenye mzani unasoma gross weight (uzito mkuu), ambao unasoma uzito wa mtungi wa gesi pamoja na mtungi mtupu.

Mzani unaweza ukawa wa kuninginiza (wenye saa) au mtungi wa kidigitali (Digital) unaosoma tarakimu.

Swali: Kwa nini kwenye baadhi ya nyumbaLUKU huisha haraka tofauti na nyumba zingine?

LUKU kuisha haraka inaweza kuwa ni matumizi ya umeme au kuwepo kwa tatizo katika mfumo wa umeme katika nyumba

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Wahandisi wa TANESCO wa 201, mteja anatakiwa kila baada ya miaka 5 akague mfumo wake wa umeme katika nyumba yake kwa kumtumia Mkandarasi anayetambulika na Bodi ya EWURA.

Maswali na Majibu

Maswali ya ulizwayo mara kwa mara

Swali: Kwa nini surveyor analipwa kuanzia shilingi 30,000 hadi 50,000 na mteja kwa ajili ya kwenda kumpimia mteja eneo lake akiwa anahitaji kuunganishiwa huduma ya umeme?

Kwa utaratibu wa TANESCO mteja hatakiwi kumlipa surveyor hela yoyote kwa ajili ya kupimiwa eneo lake na suala hili mara nyingi linatokea pale mteja anapokuwa amelipia huduma ya kuunganishiwa umeme ya shilingi 27,000. Hata hivyo, kutokana na wateja wa huduma ya umeme kuwa wengi, baadhi yao hukosa uvumilivu wa kusubiri zamu zao na kuamua kutumia njia za mkato ambapo hukutana na watu wasio waaminifu wanaowashawishi kutoa hela ili aweze kufanyiwa jambo hili kwa ucharaka. Hata hivyo, Baraza linasisitiza kuwa mteja hatakiwi kulipia gharama za tathmini.

Swali: Je, ni sawa TANESCO kujenga au kuitisha miundombinu yake katika eneo la mteja bila ruhusa?

Kwa mujibu wa Sheria ya Umeme Sura ya 131 kifungu cha 34(4) yamwaka 2019, TANESCO hairuhusiwi kujenga au kuitisha miundombinu yake katika kiwanja cha mteja bila ruhusa.

Mwenye eneo ambapo miundombinu inatarajiwu kupita endapo ataridhia anapaswa kutoa ruhusa kwa maandishi kuwa ameridhia miundombinu ya TANESCO kupita na uongozi wa Serikali za Mtaa watakuwepo kama mashahidi.

Swali: Nini kifanyike kwa nyumba yenye zaidi ya mita moja katika ulipaji wa kodi ya majengo?

Kodi ya majengo italipiwa kupitia mita moja na ikiwa mteja ametozwa kwenye mita zaidi ya moja katika nyumba moja atapaswa kuwasilisha taarifa zake katika ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili makato yaelekezwe

kwenye mita moja tu.

Swali: Ni jinsi gani mtumiaji anaweza kuangalia salio la umeme wake kwenye mita tengano za umeme (Customer Interface Unit(CIU))?

Mtumiaji anaweza kuangalia salio la umeme kwa kubonyeza code 003 kisha kitufe cha enter kwenye mita tengano (CIU) yake na atapata salio la umeme kwa muda huo.

Swali: Ni kiasi gani kwa kila nguzo moja hutozwa kwa mteja anayeomba huduma ya umeme akiwa nje ya mita thelathini kutokea kwenye miundombinu ya TANESCO?

TANESCO haiuzi nguzo kwa mteja isipokuwa bei za kuunganisha umeme kama zilivyopitishwa na EWURA mwaka 2016 zimegawanywa kwa kuzingatia umbali kutoka kwenye miundombinu ya TANESCO ili kupata gharama ya vifaa nya kufikisha huduma kwenye eneo husika.

Kwa mfano umbali wa mita mia utahitaji vifaa vingi ukilinganisha na umbali wa mita hamsini utakao hitaji gharama ndogo kulingana na uhitaji wa vifaa vichache

Swali: Rimoti ya mita ya umeme ya LUKU inapoharibika mteja akatoa taarifa, je kuna gharama anatakiwa aliye ili apewe rimoti nyingine au anapewa nyingine bure?

Kwa Mujibu wa TANESCO, kama mteja ameharibu rimoti ya LUKU atalazimika kuigharamia kiasi cha shilingi za Kitanzania 70,800/=. Kama imeharibika yenyewe atabadilishiwa bure

Swali: Kwanini mteja anapoiniza umeme kutumia remote ya kuingizia umeme mara nyingine huandika neno Error 77 na umeme hugoma kuingia?

Error 77 inamaanisha kuwa mita yako ya kwenye nguzo na rimoti yako

Maswali ya ulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

hazina mawasiliano hivyo umeme hauwezi kuingia. Mara nyingi inatoka unapotaka kuweka umeme baada ya kuisha unit zote. Jinsi ya kutatua tatizo hili ni: kwanza kuhakikisha kuwa umeme kwenye mtaa wako upo na kama nyumba yako haina umeme yaani unit zimeisha weka betri zenye nguvu kwenye rimoti yako na kisha fata taratibu zifuatazo

- i) Hakikisha swichi za nyumba yako zote zimezimwa
- ii) Washa swich moja tu ya ukutani na chomeka hiyo rimoti kisha bonyeza zero(0) ikifluatiwa na mita namba yako halafu bonyeza tena zero(0) ikifluatiwa na mita namba yako kisha bonyeza ok au enter,

Mfano mita namba yako ni
241234567 Utafanya ifuatavyo
024212345670241234567ENTER

- iii) Baada ya kubonyeza ok itaakudikia GOOD apo sasa weka umeme wako kama kawaida na utapata umeme.

Swali: Inachukua muda gani mteja kupewa huduma ya umeme pindi anapokuwa ameshalipia?

Huduma ya Umeme kwa mteja anayehitaji kuunganishiwa umeme kulin-gana na mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO ni kama ifuatavyo:

- a) Ndani ya siku 30 za kazi iwapo miundombinu iliyopo inaweza kutumika (ndani ya mita 30 kutoka kwenye nguzo iliyo karibu)
- b) Ndani ya siku 60 za kazi kama ujenzi wa njia ya umeme unahitajika (ambao siyo zaidi ya mita 100 kutoka kwenye nguzo iliyo karibu)
- c) Kama mfumo mpya wa usambazaji unahitajika kujengwa, au kama mfumo wa umeme unahitajika kuongezwa kwaajili ya kiwanda au biashara kubwa (kama hakuna mfumo wa kumuunganisha mwombaji) muda wa kumuunganisha

mteja utakuwa ndani ya siku 90 za kazi.

Swali: Iwapo gari la mteja limemwagikiwa mafuta na kuungua moto likiwa linajazwa mafuta, kwenye kituo cha mafuta, nini kinapaswa kufanya?

Kwa mujibu wa Kanuni za Petroli (Shughuli za Rejareja Mijini na Vijiji), 2020 GN 818 Kanuni Na. 26, Mto huduma anapaswa kumlipa fidia mtu au kutoa fidia ya kifaa chochote kitakachoathirika kutokana na huduma zinazodhibitiwa na EWURA baada ya mwathirika kupeleka madai yake kwa mto huduma huyo. Ikiwa mto huduma atakaidi kulipa fidia, basi mwathirika anashauriwa kufikisha shauri hilo EWURA kwa hatua zaidi.

Swali: Je ni muda gani EWURA wanatangaza bei elekezi za mafuta?

Kwa mujibu Kanuni za Upangaji wa Bei za mafuta (The petroleum Products Price Setting Rules 2020 (5(2))za EWURA, bei elekezi za mafuta zinatoka kila Jumatano ya mwanzo ya mwezi husika katika magazeti mawili ya kiswahili na mawili ya Kiingereza, ambayo yanapati-kana kiurahisi kwa wananchi. Wananchi wanaweza kupata bei elekezi za mafuta kuititia kwenye simu zao kwa kupiga *152*00#.

Swali: Nani ana wajibu wa kutengeneza bomba la maji lililoharibika kuanzia mbele ya mita kuelekea nyumbani kwa mteja?

Ni wajibu wa mtumiaji/mteja wa huduma kutokana na kanuni ya 39(1)(b) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Tangazo la Serikali namba 849 la 2020 inayoeleza;;

Ni wajibu wa mto huduma kutengeneza miundombinu (ya maji) kabla ya mita, kama uharibifu wa bomba hilo hautokani na mteja mwenyewe.



Nukuu Maridhawa

“

Kwetu sisi Baraza, haya ni mafanikio muhimu sana. Jamii inapokuwa na mwamko wa kulalamikia huduma zilizo chini ya kiwango au ukosefu wa huduma kabisa ni kiashiria kizuri, kwani kwa kufanya hivyo, watoa huduma huamka na kuchukua hatua za makusudi kutatua changomoto zinazojitokeza

-- *Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC,
Bi Stella Lupimo*

”

EWURA CCC pamoja na uelimishaji inaoufanya, imekuwa msaada katika utatuzi wa malalamiko ya wateja wetu, kwa hiyo nawapongeza na naomba tuendelee kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yetu.

-- *Meneja wa TANESCO Mkoa wa Rukwa,
Mhandisi Fedrick Njavike*